# MAISHA NDANI YA KRISTO

*THE GREEN LETTERS*
*MILES J. STANFORD*

FBC GLOBAL MISSIONS

# Acknowledgments

This translation is based on Miles J. Stanford's book THE GREEN LETTERS © 1975. We gratefully acknowledge the permission to freely translate, use and distribute this volume by the Zondervan Corporation, Grand Rapids, MI.

Translated by Grace Outreach Mission (URIRI).

# UTANGULIZI

## MAISHA NDANI YA KRISTO
## (Kiswahili The Greenletters)

Ukurasa


| | |
|---|---|
| SURA YA I IMANI | 3 |
| SURA YA 2 MUDA | 5 |
| SURA YA 3 KUKUBALIKA | 8 |
| SURA YA 4 KUSUDI | 11 |
| SURA YA 5 KUANDAA | 14 |
| SURA YA 6 KUKAMILIKA NDANI YAKE | 17 |
| SURA YA 7 KUTWAA | 20 |
| SURA YA 8 KUTHIBITISHWA | 23 |
| SURA YA 9 UWAKFU | 26 |
| SURA YA 10 NAFSI | 29 |
| SURA YA 11 KUJIKANA | 32 |
| SURA YA 12 MSALABA | 36 |
| SURA YA 13 UFEASI | 39 |
| SURA YA 14 NJIA YA UFUASI | 42 |
| SURA YA 15 KUPUMZIKA | 45 |
| SURA YA 16 USAIDIZI | 49 |
| SURA YA 17 KULIMA | 51 |
| SURA YA 18 KUENDELEA MBELE | 54 |


01-01-2011

# Dibaji

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa watu binafsi ambao walichukua nafasi yao kunihimiza, kunipatia changa moto na kunisaidia kwa kutafsiri kitabu hiki kwa Kiswahili, kusoma na kusahihisha nakala zangu za kwanza na pia kutoa usaidizi za bidhaa zilizohitajika kwa matumizi ya uandishi.

Ya kwanza ningependa kutoa shukrani zangu kwa pasta Philip Ochieng kwa himizo lake alilonipa na usaidizi wake aliyenipatia kwa shughuli ya kazi yote. Ya pili ningependa kushukuru Mike Thomas aliye nipatia Kamusi ya Kiswahili iliyokuwa muhimu sana kwangu kwa kazi hii ya utafsiri. Siwezi kusahau kushukuru Mchungaji Tim ambaye mafundisho yake yote ilikuwa gurudumu iliyo ni sukuma kufanya kazi hii.

Ningependa kuwashukuru walimu wenzangu katika shule ya msingi ya Achuth walio sahihisha kazi yangu katika kitabu hiki. Pia wale ambao tunashiriki nao katika kazi hii kama Wycliffe Juma, Joseph Juma walionisaidia sana kwa njia nyingi kwa utafsiri wote.

Ni maombi yangu kwamba kitabu hiki kitasaidia watu wengi kwa maisha yao ya ukristo.

ni mimi

Ndugu Gordon Ochieng

## MAISHA NDANI YA KRISTO
## Kanuni Za Ukuaji Wa Kiroho

## SURA YA I
## IMANI

Lengo la kitabu hiki ni kueleza kwa njia iliyo wazi baadhi ya kanuni za ukuaji wa kiroho zilizo muhimu ili kusaidia msomaji ajijenge kwenye msingi thabiti wa Biblia ndani ya kristo.

Roho mtakatifu alimwezesha Paulo kutuandikia sote kwamba,"jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani (2 wakorintho 13:5a)". Mafunzo hayo yalipendekezwa tangu mwanzo wa mfululizo wa somo hili. Kwanza, ni lazima tujikumbushe kwamba "pasipo Imani haiwezekani kumpendeza "(Wa-Ebrania 11:6a)"na Zaidi ya hayo, muhimu ni kwamba,"imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa Neno la Kristo (Warumi 10:17)". Imani yetu isipojengwa kwa msingi wa ukweli wa neno, itakuwa tu kama bahatisho, ushirikina, mawazo ama ufidhuli.

Waibrania 11:1 inaeleza mambo yote kuhusu swala hili,"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana". Imani ambayo msingi wake unatokana na Neno la Mungu inafafanua na kutupatia ushahidi wa Vitu ambavyo havionekani. Sisi sote tulianza kwa kanuni hii
Wakati tulizaliwa upya-itikadi yetu ilisimama ikielekezwa kwa ukweli wa umilele wa kifo cha ukombozi na kufufuka kwa Bwana na Mkombozi wetu Yesu Kristo (1 Wakorintho 15:1-4). Hii ndiyo imani tulianza nayo, na ni imani ile ile yafaa "tusimame",(2 Wakorintho 5:7) na "Tuishi" (Gal 2:20b)."Basi kama mlivyopokea Kristo Yesu, enendeni vivyo hivyo katika Yeye "(Wakolosai 2:6)

Kwa vile Imani ya kweli imewekwa kwenye misingi imara wa maandiko, hakika haifai tuongozwe na maono yetu.

George Mueller alisema, "maono ama mawazo hayana uhusiano kamwe na imani. Imani inatokana na Neno la Mungu. Sio maono kwa mwenye nguvu au mnyonge ndiyo yatakayoleta, mabadiliko. Lazima tuzingatie neno lililoandikwa la Biblia na siyo sisi wenyewe, sio maono ama mawazo yetu

Tena kutokea jambo kuwa kweli au la ndiyo huleta majaribio makubwa wakati tunapotembea kwa imani. Mara nyingi fikira tunayo ni kwamba "haionekani kwamba ataokolewa" "Nikiangalia dalili katika maisha yangu, sidhani kama Mungu ananipenda kweli". Lakini Mueller aliandika hivi, "Watu wengi wako tayari kuamini kulingana na vitu vinavyowezekana kwao." Imani haitokani na vitu vinavyowezekana Imani huanza wakati maono yamekoma na matarajio yetu imekosekana. Vitu vinavyoonekana kwetu hatuweki maanani. Swala kubwa ni je, Mungu amesema hayo katika Neno lake? Alexander R. Hay ameongeza kwa hili akisema,"Imani lazima ipate msingi kwa kitu cha kweli. Mpaka kuwe na hekima halisi ya kusudi la mapenzi ya Mungu. Kama si hivyo hatuwezi kuwa na Imani ya kweli. Kwa kuwa Imani sio Nguvu tunayojaribu kufanya ama kujaribu sana, kuamini ili kitu kitendeke, tukifikiria kuwa tukiamini kwa nguvu sana

kitu kitafanyika. Hayo yanaweza kuwa mawazo mema na kwa kweli sio Imani ya Biblia..

Evan Hopkins alituandikia,"Imani inataka Msingi wa Ukweli wa neno. Ufidhuli unaweza kutokana na mawazo na wala si ukweli wa neno la Mungu. Mungu anatufunulia Ukweli wa Neno ambalo Neno la Mungu hufanyia kazi." Katika msingi kama huu ndio J B Stoney anasema, "Imani ya Kweli kila mara huongezwa na upinzani Na matumaini ya uongo huharibiwa na kuvunja moyo na upinzani. Hatuwezi kusimama imara pasipo na Neno ambalo halitingiziki. Mzigo ambao Paulo alikuwa nao ni "Kujaribiwa kwa Imani yenu ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima. Katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo (1 Petro 1:7)

Tukianza kuhesabu juu ya ukweli wa Neno, Baba yetu ataanza kutujenga kwa Imani. Kutokana na kuweka imani kuu ya Bidii kwa Mungu, Mueller aliweza kusema ya kwamba, "Mungu anapenda kuzidisha Imani ya watoto wake.

Wakati mwingi hatutaki majaribio yaje kwetu kabla hatujakuwa na ushindi, ukiwa hivyo hatutakuwa na utulivu

Ingefaa tupokee majaribu hayo kutoka kwa mkono wa Mungu. Ninasema ya kwamba, majaribu, vitu vinavyo kuzuia, shida na dhiki na vitu vinavyo kushinda ndivyo Chakula cha Imani."Katika Somo hili, James McConkey aliandika: "Imani ni kuweka tumaini kwa Mungu. Kumtumainia Mungu huanza tunapoacha kujitumaini katika nafsi zetu. Kutumainia nafsi zetu kunakoma kwa wengi wetu kama kuna huzuni, mateso, maumivu, kutofaulu katika mipango na tumaini kuvunjika ndipo tunapata tukiwa katika hali ya kutoweza kufanya chochote na nafsi zetu na kushindwa. Na wakati huo tunapojifunza Somo la Imani. Tutapata maisha haya ya taabu tuliyonayo yakiendelea mbele kuwa maisha ya nguvu yenye baraka na ushindi na tutaanza kutoa huduma ambayo hatujaota kwa wakati tulikuwa tunatumainia nguvu zetu kimwili."

J. B Stoney amekubaliana na haya aliposema, "Ni jambo la maana kujifunza imani; ambayo ni kuweka tumaini kwa Mungu.Itakuwa faraja kubwa kwako na kuwa na hakikisho kwamba Kristo anakufundisha umtumainie pekee yake. Tena ni kitu cha muhimu kujua kwamba Imani inahitajika kwa kila kitu. Wenye haki wataishi kwa Imani" sio tu hali zinazotokea bali kwa kila kitu. Nina Imani kwamba bwana anakubali vitu vingi vitendeke kwa kusudi lake ili tuwe na tumaini la kumtafuta. Unavyozidi kumwona katika huzuni na mahitaji yako ndivyo utazidi kuambatanishwa naye na kuelekezwa mbali pahali hapa penye huzuni, na hadi kwake mahali alipo."Yafikirini yaliyo juu sio yaliyo katika nchi" (Wakolosai 3:2a)

Kwa kweli hatuwezi kuweka tumaini letu zaidi tunavyomjua. Kwa hivyo sio tu tujifunze hekima ya neno bali ni lazima tumjue yule ambaye hupeana uzima na kuwaweka hai."na uzima wa milele ndio huu, wakujuwe wewe, Mungu wa pekee na Yesu Kristo uliyemtuma "(Yohana 17:3.)" Na uzima huo ulidhihirika nasi tumeuona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele uliokuwa kwa Baba ukadhihirika kwetu hilo tulililoliona na kulisikia tuwahubirie na ninyi: ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba na pamoja na mwana wake Yesu Kristo na haya twayaandika ili furaha yetu itimizwe "( 2 Petro 1:2-4)

**SURA YA 2**
**MUDA**

Inaonekana vigumu kwa baadhi ya waumini wengi kutambua na kuelekeza mawazo yao kwa ukweli ambao hauwezi kubadilika kwamba Mungu hawezi kuendeleza maisha yetu ya Ukristo haraka haraka. Anatuhudumia kutoka kwa maisha yetu ya milele na kutuelekeza katika hayo ya milele Wengi wanafikiri hawapigi hatua pasipo kustawi upesi na kuzidi kuendelea mbele. Sasa ni kweli kwamba waummini waliobadilika hivi majuzi mara kwa mara huanza na kuendelea upesi kwa muda mfupi sana. Na hilo halitadumu hivyo kama kutakuwa na ustawi nzuri na mwisho kukomaa. Mungu mwenyewe atabadilisha mwendo. Hii ni muhimu kuzingatia, kama mtu ataonekana kurudi nyuma, sio vile, watu watafikiri ameanguka.

John Darby anaweka mambo wazi ya kwamba "ni njia ya Mungu kuwatenga watu wake baada ya kuanza mwendo wa kwanza ili waache kutegemea nafsi zao. Musa alikuwa na miaka arubaini alipoanza huduma yake, ilimbidi akimbilie nchi ya mbali. Paulo alikuwa na Miaka mitatu baada ya ushuhuda wake wa kwanza. Sio kwamba Mungu hakupendezwa na ushuhuda wake wa kweli. Mpaka tujitambue na kujua kwamba sisi hatuna Nguvu zozote. Lazima tujue Bwana na kumtegemea na ukomavu ndipo tutahudumia waumini wengine kwa maarifa".

Kwa maana maisha ya mkristo hukoma na kuzalisha matunda kulingana na kanuni ya ukuaji "(2 Petro 3:18,) na sio kwa kujitahidi n kufanya bidii na "ujuzi"muda mwingi unahitajika, Tusipojitambua na kuyatilia hayo maanani tutajikuta tukiwa na majonzi kila mara. Hatuwezi kusema au kufanya chochote kuzuia njia ya maendeleo ya Baba yetu kwetu.

A.H.Strong anatufafanulia,"Mwanafunzi fulani aliuliza mkurugenzi wa chuo chake kama angechukuwa muda mfupi kuliko muda mrefu uliyowekwa kwa somo lake. 'Aha Ndiyo,' Mkurugenzi alimjibu, walakini inategemea unataka uwe namna gani baada ya mafunzo." Kama Mungu anataka kutengeneza Mbao za mkaladali uliokomaa, itamchukua miaka mia Moja lakini akitaka kutengeneza unyasi itamchukua miezi sita pekee". Strong tena anatueleza kwa hekima kwamba 'Ukuaji si sawa katika miti ama wa-Kristo.

Katika miezi fulani mti inaweza kuwa zaidi kuliko miezi mingine yote ya mwaka. Kwa muda mwingine wote wa mwaka, mti inakuwa madhubuti, kama si hivyo hatuwezi kuwa na mbao nzuri za kutumia. Wakati huu ambapo mti unastawi haraka ndipo nyusi za mti zinajipanga ndani na nje ambazo ni wiki sita pekee katika miezi ya tano, sita na saba".

Wacha tueleze kwa mara ya mwisho kwamba-hakuna njia ya mkato ya kujua Ukweli! Nyota ipitayo upesi mbinguni inachukua njia ya mkato wakati inatoa mwangaza, na sio nyota ambayo inatoa nuru yake ya mara kwa mara inayotegemewa na mabaharia. Tusipofahamu kutoka kwa moyo wetu umuhimu wa muda, mara nyingi kutakuwa na hatari ya kushawishiwa kupita katika njia ya mkato tukitegemea "ujuzi"

wetu na baraka wakati mtu atajikuta katika mzunguko wa fikira na maono yatakayomtoa katika nanga ya ukweli wa Neno la Mungu.
Kulingana na somo hili George Goodman anatuandikia. “Wengine wamedanganyika wakisema wamekuwa wenye haki kamili na kupewa ukombozi kamili kwa maana wakati walikuwa wakizungumza walikuwa na furaha na ujasiri kwa Bwana, Walisahau kwamba si maarifa tunayo sasa ndiyo yanayotuhakikishia matunda na ukomavu, bali ni kuendelea mbele katika uvumilivu kwa matendo yetu na kwa kila jambo. Kuonja neema ya Mungu ni kitu kimoja. Kujiimarisha katika neema hiyo ni kitu kingine.
Ujuzi na baraka, hata ingawa ni rehema nzuri kutoka kwa Mungu lakini hazitoshi kutumainiwa wala vitufanye kupata sifa kama vile tuna hazina ya neema tunayowekewa kwa siku zijazo ama kama tumefika mwisho wa mgogoro. La Tunda huiva polepole: Kuna siku ya jua kali na siku ya dhoruba, na hali hizi zote hushiriki katika kustawi huku. Baraka itakuja baada ya Baraka na dhoruba baada ya dhoruba kabla ya matunda kusitawi na kukomaa.

Kwa hivyo kanuni ya mkulima ya ukuaji wa ukweli wa kiroho inajumuisha maumivu na pia furaha, taabu na pia msisimuko, kuanguka na kufaulu, kutofanya chochote na pia kutoa huduma, kifo na pia uhai,

Majaribu kupitia kufuata njia ya mkato yana nguvu tusipoona na kuzingatia umuhimu na mahitaji ya muda katika maisha yetu na kuweka imani yetu na kutulia kwa Bwana,”Nami niliaminilo ndilo hili ya kwamba yeye alianza kazi njema mioyoni mwenu atamaliza hata siku ya Kristo Yesu” (Wafilipi 1:6) na marafiki zangu wapendwa. Tutachukua muda mrefu! Na kwa vile Mungu anatuhudumia kwa ajili ya uzima wa milele, kwa nini tujali muda ule utakaohusishwa?

Graham Scroggie anahimiza; “Maisha ya kiroho huwa ni kuendelea polepole. Ukuaji wote unaendelea hatua kwa hatua, tukiwa na kitu kizuri cha kufanya kwa ustadi kinachukuwa Muda mrefu Kukitengeneza Kitatoka katika kipimo kimoja hadi kingine,mara thelathini,mara sitini, na mara mia Moja. Ni kutoka hatua hadi hatua: kwanza ni kijani baadaye suke na baadaye mbegu iliyokomaa inamea kutoka kwa kijani. Inabadilika kila siku, haya yana hali mbali mbali! Kuna siku ambazo ni kuu, siku ya kukata kauli ya vita katika maisha yetu, siku za migogoro katika historia ya kiroho yetu, siku za ushindi katika huduma zetu za Ukristo, siku ambazo mkono wa kulia wa Mungu uko juu yetu. Lakini kuna siku tuko wavivu, siku ambazo zinaonekana dhahiri kuwa bure, wakati hata maombi hata huduma takatifu inaonekana kuwa mzigo. Je, katika hali yoyote tunayojikuta, tumebadilishwa kuwa wapya? Ndio, kwa maana hali yoyote tunayopitia inatufanya tugundue kumhitaji Mungu lazima ichangie kwa ustawi wa Roho. Isipokuwa tunamnyima Bwana nafasi aliyetununua”.

Tunaweza kuyakumbuka majina ya watu tunaowajua kuwa na imani ambao Mungu aliwafanya wakakomaa na kuwatumia kwa ajili ya utukufu wake majina kama ,Pierson,Chapman,Tauler,Moody,Goforth,Mueller,TayloWatt,Trumbull, MeyerMurray,Havergal,Guyon,Mabie,Gordon,Hyde ,mantle,McCheyne, McConkey,Deck,paxson,Stoney, Saphir,Carmichael na Hopkins. Nusu ya idadi ya hawa ilikuwa miaka kumi na mitano baada ya kuweka maisha yao kwa huduma kabla ya kumjua Bwana Yesu katika maisha yao, na kukoma kujaribu kumfanyia kazi na

kuanza kumruhusu Yesu awe kila kitu ndani ya Maisha yao, na kufanya kazi kupitia kwao. Hili lisiwe jambo la kuturudisha nyuma katika hali yoyote, bali litusaidie na kutulia na mitazamo ya milele, kwa Imani “Tambua (Kutambua ambako nami nimetambua Yesu Kristo--------Kaza (Kukaza) mwendo kuelekea pahali pa tuzo ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu”) (Wafilipi 3:12b, 14)
Kwa hakika sio kufikiria tu hali tunayoipitia inayoendelezwa kiroho, baraka au hata wakati wa hali mbaya; lakini yafaa ikumbukwe kwamba haya yanayochangia yote kwa ujumla, na hata yoyote ya muhimu, Inachukua muda mtu kujijua mwenyewe; inachukua muda wa milele kujua Bwana Yesu Kristo ambaye hana mwisho. Leo ni siku ya kuweka mkono kwenye kifaa cha kulimia, na hatimaye uelekeze Moyo kwenye lengo la Yesu la mwisho kwetu. “ili nimjue yeye, na uwezo wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake”(Flp 3:10)

“Mara kwa mara vitani, asema Austin –Sparks,” “Twaenda kwa bwana,na kuomba, na kumlilia, na kuomba usaidizi wa kushinda, nguvu za kushinda, ujuzi wa ukubwa dhidi ya nguvu za uovu na kifo ,na tumaini letu ni kwamba kwa kiasi Bwana anaenda kuingilia kati kwa nguvu zake kuu na kutuweka pahali pa ushindi na nguvu za kiroho kama vile katika matendo ya mitume. Ni lazima tuwe na hili lililorekebishwa akilini mwetu. Kile Bwana hufanya ni kutupanua tuweze kumiliki. Anatuweka kupitia majaribu, katika hali tunazopitia, anatupeleka kupitia katika njia inayo maanisha upanuzi wetu wa kiroho, na mwenendo wa kiroho kuwekwa kwenye matendo kwa hivyo tunachukua pahali pakubwa kwa hiari “Sitawaondoa kutoka mbele yako kwa muda wa mwaka mmoja; nchi yako isije ikabaki ukiwa, na mnyama ambaye ni muovu aongezeke dhidi yako. Kidogo nitawaondoa mbele yako, hadi wewe utakapoongezeka” (Kutoka 23:29,30)

“Siku moja katika jumba la ushirikiano, Waziri mkuu wa Uingereza Disraeli alitoa hotuba nzuri ya kuvutia kwa ghafla usiku huo huo rafiki yake akamwambia,’Lazima nikueleze jinsi nilifurahia mazungumzo yako yaliyoyokuwa ya ghafla. Yamekuwa akilini mwangu siku nzima! “bibi” Disraeli akakiri,’hayo mazungumzo yangu ya ghafla yamekuwa kwenye akili yangu kwa muda wa miaka ishirini!”

## SURA YA 3
## KUKUBALIKA

Kuna maswali mawili ambayo kila mtu ambaye ameamini atafute majibu haraka iwezekanavyo. La kwanza ni, Je, nimekubaliwa na Mungu kikamilifu? Na, kama hivyo, ni kwa njia ipi amefanya hivyo?Hii ni muhimu sana. Ni uharibifu gani ambao daima hupenyesha maisha ya mtu,mdogo au mzee, tajiri au masikini, aliyeokoka au ambaye hajaokoka,ambaye hana uhakika wa kukubaliwa, hata katika kiwango cha ubinadamu.

Bado watu walioamini wengi, wawe'wenye kupambana'au wasio pambana na maisha'wanapita na kujenga juu yake: "Kuwa tumetunukiwa kutunzwa kama watoto na Yesu kristo kwake mwenyewe kulingana na mapenzi yake ya hiari, kwa sifa za utukufu wa neema yake, katika hiyo ametufanya tumekubalika katika kupendwa" .(Waefeso 1:5,6)

Yeyote ambaye ameamini amekubaliwa na Baba, kupitia imani, tuna amani na Mungu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo "(Warumi 5:1). Amani ni Mungu kuwa upande wetu kupitia kwa mwanawe mpendwa -----Kwa hili, amani yetu itaimarishwa. Mungu ana uwezo wa kuweka amani nasi kupitia kwa damu yake msalabani" (Wakolosai 1:20). Na ni lazima tusisahau kwamba amani yake imepatikana pekee yake kwa kazi ya msalaba, pasipo kabisa na kitu kingine chochote kile kwetu au kutoka kwetu kwa vile "Mungu amependekeza upendo wake kwetu kwamba, wakati tulikuwa tungali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajili yetu"(Warumi 5:8.)

Imani yetu huwa ni kule tunakoelekeza mawazo yetu yote, wakati inapoanza kutulia katika ukweli huu wa ajabu. Huu ndio mvutio imara ambao wengi wa wale walioamini wanahitaji kwa sasa. Karne moja iliyopita, J.B.Stoney aliandika:"Mungu mbarikiwa habadiliki wala hageuzi njia ya kukubalika ambayo ametupokea nayo kwasababu ya kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Ole Wetu! Tunamwacha Mungu katika hali ambayo anaendelea kuwa upande wetu jinsi ilivyoandikwa katika Warumi 5:1-11. Wengi hudhania kwamba wanatambua dhambi, kwa ajili ya sababu hii, ni lazima watafute zaidi kukubalika na Mungu."Ukweli ni kwamba Mungu hajabadilika. Jicho lake limeelekezwa kwa kazi iliyomalizwa na Kristo kwa walioamini. Wakati hauenendi katika Roho basi uko katika mwili: Umemgeukia yule mtu wa zamani ambaye alisulubiwa msalabani ( Warumi :6:6) Umerejeshwa kwa ushirikiano, na hivyo, upate kibali kutoka kwa Mungu bila Kubadilika na asiyebadilishwa. Wakati dhambi zinajitokeza na kukaribishwa kuna hofu ya kwamba Mungu amebadilika. Hajabadilika, lakini ni wewe mwenyewe umebadilika. Hautembei katika Roho bali katika mwili. Hujihoji wewe mwenyewe ili usongezwe tena karibu na Mungu." "Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"(Mat. 26:28). Lakini iwapo dhambi zako hazijaondolewa, lini zitaondolewa?" "Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapana toleo tena kwa ajili ya dhambi "(Wahebrania 10:18). Mungu ametekeleza mapatano: Yeye hubaki kuwa kweli kwa hilo. Ole! sisi huenda mbali na hilo; na tabia ni kuchukulia kwamba Mungu mwenye baraka ametugeukia. Kwa hakika yeye hukumu mwili iwapo hatuenendi mbali na yeye, lakini Yeye haendi mbali na

pendo ambalo amelionyesha kwa mwana mpotevu, na tunakuta kwamba wingu la kutembea katika mwili linapoingia, limepita, pendo lake, jina lake libarikiwe halijabadilika.

Msingi wa Mungu lazima uwe msingi wetu ili tukubalike. Hapana mwingine. Sisi "tumekubalika katika penzi," Baba yetu ameridhika na mwanawe mpendwa kwa niaba yetu.,na hapana sababu ya sisi kutokuwa hivyo. Kutosheka kwetu kunaweza kutoka kwa kutulia katika Kutosheka kwake. Ni kutoka kwa Mungu hadi kwetu, wala si kutoka kwetu hadi kwa Mungu. J.Darby alikuwa wazi kwa hili: "Wakati Roho Mtakatifu ananena na mwanadamu, Yeye haneni kutoka kwa yale mwanadamu anayo kwa Mungu, Lakini kutoka kwa yale Mungu anayo kwa mwanadamu. Nafsi zanena kutoka kwa yale yako ndani zenyewe kama vile Mungu aweza akazikubali. Hawezi akakubalia vivyo hivyo; Unatafuta haki kutoka kwako mwenyewe kama msingi wa kukubaliwa na Mungu. Hauwezi kukupa amani huku ukiwaza kwa njia hiyo.

Roho mtakatifu daima huwaza kulingana na vile Mungu alivyo, na hii huleta mabadiliko yote katika nafsi yangu. Si kwamba ninachukizwa na dhambi zangu; hakika yawezekana kuwa nimekuwa nikitembea vizuri; Lakini "Ninajichukiza mimi mwenyewe". Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu huwaza; anatuonyesha jinsi tulivyo na hii ndiyo sababu moja inayomfanya mara kwa mara anaonekana mgumu na hapeani amani kwa nafsi, jinsi hatujatulizwa hadi tutakapoyapitia hayo, katika nafsi zetu, kutambua kile tulicho.

"Hadi wakati ambapo nafsi itafika kiwango ambacho Yeye hataipa amani:----- Hawezi kamwe ;ingekuwa ni kuponya jeraha kidogo tu, Nafsi itaendelea hivyo hadi wakati itakapopata kwamba hakuna chochote cha kuegemea kwacho bali ni uzuri uliotolewa kwa Mungu; halafu, "Mungu akiwa upande wetu, ni nani atakuwa kinyume chetu?" (Warumi 8:31 b)

La kuhuzunisha, siku hizi waamini wengi huwaza kinyume—Kutoka kwao hadi kwa Mungu.Wakati Kila kitu kinatendeka vema, na Mungu kuonekana kuwa mwenye kubariki, basi ndipo hapo wanadhania kwamba anawapenda na kuwakubali. Lakini wakati wana mashaka, na kuonekana kukiwa na ugumu, basi wanajihisi kana kwamba hawaipendwi na kuwakubali hili linaionekana kwa namna gani? Hakuna chochote kuhusu sisi kitakachokupendekeza kwa Mungu, kukubalika kwetu huwa katika Kristo, aidha ukweli kwamba ukuaji wetu wa kweli wa Kiroho huja kupitia ukavu na hali ambazo ni ngumu. Mshukuruni Mungu ametupa Kibali katika mwanawe, na juu ya ukweli huu tutulize imani yetu. Na katika kuhesabiwa haki, kukubaliwa ni kwa njia ya neema pekee.

Katika ubora wake, Warumi, mstari hadi mstari, Wm.R.Newell ameleta fikira za kupenyeza kuhusu neema hii. Kwa kuwa hapana chanzo katika kiumbe kwamba ni kwa nini neema ionyeshwe, kiumbe ni lazima kifanywe kwa kujaribu kutoa kiini kwa Mungu kwa hima yake" "Amekubalika katika Kristo, ambaye ni msimamo wake!" "Hayuko katika majaribio". "Kama maisha hayako mbele ya Mungu: Alikufa msalabani, na Yesu ni maisha yake". "Neema, wakati ilitolewa, haikuondolewa: kwa maana Mungu alijua mahitaji yote mbeleni; Kitendo chake kilikuwa mbali na vingine, sio

kuvitegemea”.“Kuamini, na kutoa idhini ya kupendwa tulipokuwa tungali hatustahili, ndiyo siri kuu.

“Kukataa kutoa ‘Kauli’ na ‘Ahadi’; huku ni kutumainia “Kutarajia kubarikiwa, ijapo kutimiza na zaidi ya kutostahili”.“Kutegemea mkono wa kurudi wa Mungu kama alama ya ukarimu”.“Kuwa na ‘tumaini’ la kuwa bora “(kukubalika) ni kukosa kujiona katika Kristo pekee”.“Kukosa tumaini ndani yako ni kujitumainia wewe mwenyewe.“Kushushwa moyo ni kutokuwa na imani-kulingana na kusudi la Mungu na mpango wa baraka kwako”.

“Kuwa na kiburi ni kuwa kipofu! Kwa maana hatuna msimamo mbele ya Mungu ndani mwetu”.“Kukosa baraka mbele za Mungu, kwa hivyo hutokana na kutoamini, wala sio kukosa kujitolea kwa bidii”.

“Kuhubiri kujitolea kwa bidii kwanza na pili baraka ni kugeuza mpangilio wa Mungu, na kuhubiri sheria, sio neema. Sheria imefanya baraka za mwanadamu kutegemea kujitolea kwa bidii;Neema huongea sio ya haki, baraka isiyo ya masharti. Kujitolea kwetu kwaweza fatia, lakini haifanyiki hivyo – kwa kipimo kizuri”.

Tumekuwa waoga kweli kuamini Mungu? Kuna hata baadhi ya watu ambao wamekuwa waoga kuwaruhusu wengine kumuamini kweli? Ni lazima tusisahau kwamba

“Njia za Mungu siyo njia za mwanadamu. Kwa wanadamu wengine mashaka yasiyobadilika ndiyo mwiba tuu kwa matendo, na dini nyingine na elimu ya Roho, na akili vinaegemea kwa woga kuwaweka wafuasi katika njia. Hofu, pia ina nafasi katika Ukristo, lakini Mungu ana mvutio wa hali ya juu na wa kutenda kuliko hofu, na mojawapo ya haya ni upendo. Wakati mwingi, hofu baada ya kitambo kidogo huzaa tu ulegevu, lakini upendo hustawi kwenye upendo. Kumuahidi binadamu ukweli wa hali yake kwaweza onekana, kwa kiwango cha binadamu, kama kucheza na moto; Wale ambao wanatambua kwa kindani juu ya neema hawaendelei katika dhambi. Zaidi ya hayo hofu huzaa utii wa watumwa; upendo huamsha usikivu wa wana”. J.A.Sanderson Jr,” Kwa maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?”(Wakorintho 14:8). Hadi mkristo atakapokuwa na uhakika, hali yake ya ukweli kulingana na Neno, haendi kuwa na msimamo,”Basi simameni”(Waefeso 6:14a)

Na Bwana wetu Kristo Yesu mwenyewe,na Mungu Baba yetu aliyetupenda akatupa faraja ya milele na tumaini jema, katika neema, awafariji mioyo yenu, na kuwafanya imara kwa kila neno na tendo jema” (2 Wathesalonika 2:16,17)

“Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote, Mungu hufanya kazi pamoja na wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi lake, Maana wale aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake” (Warumi 8:28,29). Hapa kuna “wema” ambao Mungu hufanya nao kazi mambo yote – kusudi lake la asili la kutufanya sisi katika mfano wake, ambao umewekwa na kudhihirishwa katika mwanawe, Kristo ambaye ni uhai wetu. Kujitolea kwa Paulo kwa waliobadilishwa upya ni ,”Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu “(Wagalatia 4:19)
Siri ya wazi ya ukuaji Kiroho wa afya ni kutambua na kutulia kwenye ukweli huu jinsi ulivyoelezwa katika Warumi 8:28 na 29.Wakati tunaona kwamba mambo yanafanyika pamoja hutuweka zaidi na zaidi kama Bwana Yesu. Hatutazuiliwa na kuhangaishwa wakati baadhi ya hivi “Vitu” ni vigumu, si rahisi kuvielewa, na mara nyingi vimebeba chanzo cha maafa. Tutaweza kutulia katika Bwana wetu Kristo Yesu na kusema kwa baba Yetu,”Mapenzi yako yatendeke “. Na hisia zetu imara za imani zitakuwa. “Tazama, ataniua; sina tumaini ila hata hivyo nitadhibitisha njia yangu mbele yake” (Ayubu 13:15). Hili ndilo jaribio la kutuingiza katika kukomaa kiroho.

“Lakini sisi sote, nyuso zetu zikiwa wazi kana kwamba tunaangalia kio cha utukufu wa Bwana, twabadilishwa tufanane na mfano huo huo, toka utukufu hadi utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho” (2Wakorintho 3:18) Kitu kimoja cha kutambua ni kusudi gani kwa Mungu kwa maisha yetu, na kingine cha kujua ni "Njia gani” ya ndani yake hapa na sasa. Mojawapo ya njia mwafaka ya Mungu katika mipango yake ni kutofaulu kwa hivyo waamini wengi wamechanganyikiwa juu ya ukweli wa kutofaulu maishani mwao, na wataenda kwa urefu kujaribu kuficha, kupuuza au kulieleza kwa jinsi ya akili ya kibinadamu, na wakati wote wanajaribu kwenda kinyume na mbinu ya kipekee katika mkono wa Mungu kutugeuza sisi kwa mfano wa mwana wake.

Kushindwa ambako kunatuhusu katika maisha yetu ya kikristo na huduma, kunakubalika na mara nyingi hutekelezwa na Mungu ili kutugeuza kabisa kutoka kwa usisi hadi kwa chanzo chake kwa ajili ya maisha yetu-Kristo Yesu, ambaye hashindwi. Furahi, rafiki mpendwa, kutaka hitaji lako na njaa ya moyoni, kwa maana Mungu asema, “Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa ” (Mat 5:6) kama vile sisi, katika hitaji letu hafifu, kwa uthabiti na upendo twaangalia kwa Bwana wetu Yesu aliyefichuliwa kwetu katika Neno Roho Mtakatifu atabadilisha msimamo wetu na chanzo chetu polepole na bila kutumia nguvu kutoka kwa usisi hadi kwa Kristo-kwa hivyo kwa kila mmoja wetu itakuwa, “Si mimi bali Kristo”

Mungu ana sheria ya kiasili katika nguvu ambazo zinatekeleza kwa kuwa tumebadilishwa kutoka pale tumeelekeza matakwa yetu na upendo. Hawthorne ameleta ukweli huu katika “hali ya macho makavu”. Halafu tena fikiria juu ya ujerumani miaka iliyopita, imejaa mahitla wadogo wadogo yote kwa ajili ya hamaki ya kujitolea kwa bidii hadi kwa kukaripiwa kwa pili kwa njaa ya karatasi! Hapa ni vitabu vyetu vya nchi wa kusimama, redio, runinga na picha za kanda zote zimechangia katika kutupatia kizazi kinachoibuka cha vijana vya utumishi kwa wote, wachungaji ng’ombe, magenge ya majambazi n.k. Na waamini nao je? Iwapo tutavutwa na dunia hii ya

kisasa iliyojaa uovu, tunakuwa wa kidunia sana; Iwapo tutakuwa wa kudokezwa na tuishi kwa usisi, tutakuwa wa kujiangalia tu zaidi na zaidi, lakini tukimwangalia Yesu Kristo, tutakuwa kama Yeye zaidi na zaidi. Norma Douty aandika “Iwapo niko kama Yeye, basi Mungu katika neema yake lazima afanye, na jinsi ninavyotambua hivyo, vivyo hivyo ndivyo mtakombolewa kutoka katika utumwa mwingine. Weka chini jitihada na useme, siwezi kufanya, vile ninavyoendelea kujaribu zaidi, ndivyo ninavyotoka katika mfano wake. Nifanye nini? Aha, Roho Mtakatifu asema, Hauwezi kufanya hivyo; wachana nayo; na uondoke kabisa. Umekuwa ukijaribu, umeshindwa, toka ndani yake na uketi, na unapoketi hapo, mtazame Yeye, mwangalie Yeye Usijaribu kuwa kama Yeye. Badala ya kuyaacha hayo yote yajaze fikira zako na moyo wako, wacha Yeye ajaze yote. Mtazame tu kupitia kwa neno. Njoo kwa neno kwa kusudi moja na hilo ni kukutana na Bwana. Sio kuacha fikira kujazwa na vitu kuhusu Neno takatifu, bali njoo kwake kukutana na Bwana. Lifanye liwe chombo, sio malipo ya wanachuo cha kibibilia, bali la ushirika na Kristo.Mtazame Bwana.

Wewe wasema, nilinganishe, niumbe kwa ajili yako.
Nyosha mikono yako tupu, na uwe wewe;
O nafsi isiyotulia, inafanya lakini inanizuia,
Na kusudi lenye ujasiri na nia madhubuti
Tazama Maua ya kiangazi chini ya jua,
Katika unyamavu utukufu wake mkuu wautazama
Na kwa utamu huu huu neno lake kuu limefan
Na kutulia katika uchangamfu wake yanatandua
Ndivyo utamu na furaha ya kiungu
Yako, ya ikupendeza, Na kazi ni Yangu
-Ter Steegen

“Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutoka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema” (Wafilipi 2:13) Na “Kusudi lake jema” ni lipi? “Unalotekeleza” ndani yetu? Anafanya yote kwa pamoja kwa kusudi lake moja;
“Ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti” (2Kor 4:11). Na huu ndio uzima “Kwa maana kwangu kuishi ni Kristo” (Filipi 1:21). Hii ndiyo huduma;

“Palikuwa na wayunani kadhaa wa kadhaa---------wakisema, Bwana sisi tunataka kumwona Yesu” (Yohana12: 20.21)

# SURA YA 5
# KUANDAA

Tunapotambua mpango wake wa milele na kusudi lake kwetu, ukiongeza njia Yake ya kuandaa na jinsi hiyo hadi mwisho,kuna kutulia na tumaini.Inatokea kwamba sehemu muhimu ya Mungu katika ukuaji ni hitaji. Bila mahitaji ya kibinfsi, hatuwezi kufika mahali popote katika maisha yetu ya Ukristo. Sababu inayomfanya Mungu kutengeneza na kuruhusu mahitaji yetu ni kugeuza sisi sote kutoka kwa yale yote yaliyo nnje ya Kristo, na kutekeleza kwake pekee. “Si mimi bali Kristo”

Kwa maana kukua kwetu na huduma yote ni ya muhimu kwamba tunaona na kuelewa kanuni hii, ambayo J.B.Stoney ameiweka katika sentensi; “Nafsi haihifadhi ukweli katika nguvu za kudumu lakini jinsi inavyohitajika.”Na kwa ukuaji, wetu, mahitaji yanatufanya kufikia na kuwa sawa kupitia imani, kutoka kwa Bwana wetu Yesu, tunayohitaji. Na katika swala la huduma,katika kushuhudia na kuwasaidia wengine, ni lazima tukeshe na kungojea njaa, moyo wa kuhitaji, kama tutakuwepo na tunda la kudumu.Tena Stoney asema, “Thamani halisi ya kitu chochote kile itajulikana tu wakati hicho kitu kitahitajika. “Hekima na elimu ya elimu zote havifafanui Mungu; Yeye hujifunua kwetu kupitia mahitaji yetu: Sharti humtafuta Mungu. Nina tashwishi iwapo tumeshawahi kujifunza kitu chochote madhubuti isipokuwa tumejifunza vivi hivi.”

Katika uwazi huu, mahitaji yetu hayana thamani yoyote! Lazima tufuate ukweli kwamba bila njaa ya kiroho, hatuwezi kupata lishe bora kutoka kwa Bwana Yesu Kristo. Kutokana na hali ambazo tumepitia za kibinafsi, Mathayo 5:6 lazima iwe na maana kubwa kwa kila mmoja wetu – “Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.”Mara kwa mara walioamini wanashauriwa na hata kushinikizwa kukua kabla hakujawa na hitaji la kupita kiasi, kabla hakujawa na njaa halisi ya kiroho. Na, la huzunisha kusema, katika hali nyingi za njaa ya kweli ya moyo, chakula kichache cha kiroho hutolewa. Sababu moja kuu ya bidii ya uinjilisti na kazi ya kibinafsi kuwa chache au bila kitu ni kwamba ukweli unasukumwa kwa “asumbuliwaye” kuokoka kabla hajajua kwamba amepotea. Hivi karibuni kazi itakuja kuwa bila faida ila tu nguvu kuu za kusadiki kuwa mwenye dhambi zitamfanya aliyepotea kufikia na kukamata imani ya kibinafsi, na kupata hitaji lake kamili katika mkombozi.

Watchman Nee aweka vitu vya kwanza mbele kwa kusema, “Bwana hatuweki hapa kwanza kuhubiri, au kumfanyia kazi yoyote ile. Kitu cha kwanza ambacho ametuelekeza kukifanya ni kuunda njaa ndani ya wengine.
kupeleka watu kuwa katika hali ya kuona njaa. Hiyo njaa itaundwa, na hiyo njaa yaweza kuundwa tu kupitia kwa wale ambao wamebeba maono ya Mungu.

Katika kuandaa, kuna kubomolewa kabla ya kujengwa. “Njooni tumrudie BWANA; maana Yeye amerarua na Yeye atatuponya; Yeye amepiga,na Yeye atatufunga jeraha zetu.” (Hosea 6:1). Hii yahusu kukua pamoja na huduma. J.C.Metcalfe kwa uaminifu aandika; “Ni jambo la faraja zaidi kujua kwamba ni wale ambao wameweka sawa sawa vina vya kutofaulu ambao umepeanwa kwa wale walio na vipawa, ambao wamepata mafunzo ya hali ya juu, au waliosafishwa.

“Bila hali mbaya tunayopitia kwa kupungukiwa kwao na umaskini ambao kwa mtu ambaye amegundua kitu cha kadiri ya upungufu wake kuwa mstahimilvu kwa unyonge wa fikira za wengine. Mtu huyo tena ana hekima iliyo bora zaidi utunzaji wa mapenzi ya Mchungaji Mkuu, na uwezo wake wa kuponya yule amekuja kwa kunyenyekea kuamini ndani Yake na Yeye pekee. Kwa hivyo, hakata tamaa kwa urahisi kwa ajili ya wengine, lakini huangalia kupita kiasi cha dhambi, kuwa na nia, na upumbavu, hadi kwa ukuu wa upendo usiobadilika. Bwana Yesu hatoi shutma. “Uwe mchungaji wa kondoo wangu------kwa kondoo wangu; baada ya kusikia matamshi ya Petro ya ujasiri kuonyesha uaminifu, lakini anapeana baada ya kukosa kutimiza ahadi zake na kulia kwa uchungu katika mitaa ya Yerusalemi.”

Ndio, lazima kuwe na kujiandaa kwa kindani, kweli na kwa urefu iwapo kutahitajika uhalali-iwapo maisha yetu ni ya kuelekezwa kwa Kristo, kazi zetu zikiongozwa na Roho Mtakatifu, na huduma zetu zikimtukuza Mungu. Punde si punde Roho Mtakatifu huanza kutufanya tujue shida zetu kuu kama walioamini- tofauti nyingi zilizoko kati ya ubinafsi na Kristo, “Kuna wafanyi kazi wengine kando ya wale wanaotaka msamaha-huhesabiwa haki-kwa wafanyi kazi wa utakazo wa kibinafsi- baada ya kutolewa kwa nguvu za Adamu wa zamani:na kwa hivyo, hata na kwa wale ambao wanatafuta wokovu, Kristo ahaidi, na ukuu huu “ninaweza.” (Mat 11:28-30). Kuna uwezekano mkubwa wa mtu, baada ya kupata utulivu na haki katika Kristo, kuingia katika hali ya hitaji la kindani kulingana na utulivu wa utakazo. Twafikiri kuwa hatutakosea ikiwa twasema kuwa hii imekuwa ni hali ambayo karibu kila aliyeamini amepitia ambaye amewahi kuishi”(P.B.Power)

Kuandaa kwake kwingi katika maisha yetu ni pamoja na kuanzisha pambano hili- mtazamo wetu wa kibinafsi jinsi ulivyo, na kujaribu kujiondoa kutoka kwa nguvu zake mbaya na ushawishi. Kwa maana hakuna tumaini la kuendelea kukua katika Bwana Yesu iwapo tungali chini ya mamlaka ya maisha ya binafsi, ambayo nani yake “halikai neno jema.”(Warumi 7:8a)“ Sio katika mwili tunaweza kuendelea kukaa katika uwepo wake, bila kujali mazingira yetu na yale tunayoyafanya.

Sio wakati tunapomtumikia na hamu ya kurudiarudia ndio nafsi zetu hukua na kustawi: Si wakati ambao hatujali ndio hatunyeshewi na uwepo wa Bwana. Ni wakati tumeingizwa kabisa, kusafishwa, na kurudiwa: wakati upendo wa kibinafsi na dunia imetukomea kabisa, kwa tunajifunza kukaa katika kuguzwa na Yeye kila wakati, na pahali popote pale au mazingira.”

Thamani ya kung’ang’ania kuwekwa huru sisi wenyewe kutoka kwa maisha ya Adamu mpya, maisha ya Kikristo, ni kutambua hatimaye kwamba ni bure. Kutofaulu kwa kuvunja moyo kwa kibinafsi katika kila kiwango chochcote cha maisha yetu ya Ukristo ni maandalizi ya Baba wetu kwa kufaulu kwake kwa niaba yetu. Huku kuunda kwake kwa kutokujali baadaye atatuleta kwa ahadi yake ya kweli ya Wafilipi 1:6, “Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye alianzisha kazi njema mioyoni mwenu Ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.”Kazi Yake “ Njema” ndani yetu inaanza kupitia kutofaulu; na hii inajumuisha vidokezo vyetu maalum, ambavyo vinaendelea mbele kwa kufaulu kwake, kupitia kufanya kwake, wala sio wetu. “Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kulitimiza kusudi lake jema.” (Filipi 2:13)

Hakuna tashwishi ila kwamba sote tulianza katika neema ya kweli, na ni lazima tuendelee na tufikie kwa hilo tu: “Katika ungwana huo, Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kungwa la utumwa.” (Wagalatial5:1).

Charles Trumbull alisema; “Maisha yasiyo na nguvu si maisha yasio na nia. Tunatumia nia yetu kuamini, kupokea, wala sio kuweka nguvu katika kujaribu kukamilisha tu yale awezayo kutenda. Tumaini letu la ushindi dhidi ya dhambi sio ‘Kristo ukiongezea jitihada’ bali ‘Kristo ukiongezea kupokea kwangu.” Kupokea ushindi kutoka kwake ni kuliamini Neno Lake kwamba pekee kupitia neema Yake Yeye ni, wakati huu, anatuweka huru kutoka kwa utawala wa dhambi. Na kumwamini Yeye katika njia hii ni kutambua kwamba anatufanyia sisi yale hatuwezi kuyafanya sisi wenyewe.

“Tulijifunza kanuni hii wakati wa kuzaliwa kwetu kiroho, na yaonekana kwamba wengiwetu watakiwa kujifunza zaidi na zaidi kwa ajili ya ukuaji wetu wa kiroho na huduma. Msiogope msihofu wapendwa; shikenina muwe imara kwa jambo la kusudi lake kwa ajili yenu katika Kristo, na Yeye atawapeleka hatua kwa hatua kwa uaminifu hadi kwenya maandalizi yaleyanayotakikana-Yeye atafanya. Wakati atakuwa na uhakika wa kusudi utakuwa vile vile na uhakika ma maandalizi. Vivyo hivyo kumbuka kwamba Warumi 8:28 na 29 yaandamana, na mshuku Yeye kwa ajili ya Wafilipi 1:6. “Bwana anatukuka katika wale ambao mioyo yao imemuelekea kwa vyovyote vile, kupitia barabara yoyote, kwa lengo ambalo ni Mungu mwenyewe. Mtu ambaye hivi sasa amekumbukwa asema, kwa njia yoyote! Hapa kuna barabara ngumu: barabara ambayo imeviziwa na maadui, lakini shauku kwa ajili ya lengo itamshikilia imara katika njia. Ni binadamu ndiye anayekosa shauku ya kumtambua ambayo itabadilishwa kwa urahisi na kuwa kinyume. Katika barabara hiyo Mtu Kristo Yesu amekwisha tangulia, na katika kila sehemu ametushindia. Haifai tupande juu; tunapitia katika gari lake la ushindi. Kila adui ameshughulikiwa vilivyo; kila adui ameshindwa; hakusalii chochote ambacho hakijawekwa chini ya nyayo zake, na hakubaki chochote ambacho katika sayari hii kitamshinda mwana wa mwisho wa Mungu ambaye amechukua mkono wa Bwana na alisema: “Bwana nifikishe mahali ambapo Wewe Upo, katika wema wa damu ambayo Wewe tayari umechukua katika ushindi.” Kuna utukufu mkuu wa Bwana katika utulivu, kutembea kwa ujasiri katika siku ya mateso, siku ya hofu, wakati ambapo vitu ambavyo vimetuzunguka vitatikisika na kutetemeka.”(G.P)

## SURA YA 6
## KUKAMILIKA NDANI YAKE

Tunaendelea kushughulikia ukweli wa kimsingi, kwani maisha yaweza yakawa mabaya kuliko Shina Lake, chanzo chake. Ujana na kutokomaa kwaonekana kwanza na kuwaza baadaye, kwa wakati mwingi. Kukomaa kumejifunza kuchukua muda wa kuthamini ukweli. Mkulima wetu mvumilivu anatupa muda kwa hiari na kujifunza ukweli wa umilele, ambao bila huo hatuwezi kukomaa

Bwana wetu Yesu kwa wakati mwingi hutumia ukweli wa asili kutufundisha ukweli wa kiroho kwa kina. Yeye kwanza hutufundisha kuhusu asili yetu, maisha ya mwana ya Adamu kabla ya sisi kumaizi na kufurahia uzuri wetu wa kuwa kiroho upya, maisha ya Ukristo.Hii yahusisha chanzo muhimu cha kanuni-“Kwa mfano wake.”Kila aliyeamini hujifunza kwamba yu mkamilifu katika Adamu-yeye alitoka kwake;Yu kama yeye. “Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi.”(RUM5:19a) “Kwa maana najua kuwa ndani yangu (yaani ndani ya mwili wangu), halikai neno jema.”(RUM7:18a), wakati, kupitia kwa kuanguka kwetu na juhudi zetu,Yeye ametufunza kuhusu asili, tutakuwa tayari kujifunza chanzo cha kiroho. “Kwa kutii kwake mmoja wetu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.”(RUM5: 19b). “Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Nanyi mmetimilika katika Yeye.”(Kol 2:9,10a)

Kuna jinsi mbili kwa hiki chanzo cha kanuni. Kwanza, Bwana yesu ndiye chanzo cha maisha yetu ya ukristo-tulizaliwa katika Yeye; Mungu ametufanya tumetimilika ndani yake. Huu ukweli ni kwamba tuushike kwa imani, ni kweli katika mmoja wetu. “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya……”(2KOR 5:17a) Pili, namna tunavyoshikilia kwa ukweli huu kwa imani, tumeletwa katika ukweli wake wa kutendwa siku baada ya siku katika hali zetu tunazopitia. Pole pole tunapokea lile ambalo lilikuwa tayari ni letu. Jambo la muhimu ambalo latupasa kulitambua na kuwa hakika nalo ni kwamba yote ni yetu, tumekamilika ndani yake sasa. Ukweli huu unatuwezesha kutulia huku akifanya katika uvumilivu tabia yetu kwamba maisha yetu ambayo yamefichwa na Kristo ndani ya Mungu.

“Kuendelea mbele ni kupanda tu katika hekima, hekima ya kiroho, juu ya yale tumeshikilia mwanzoni. Ni kama ngazi ya kupanda. Ngazi ni neema. Hatua ya kwanza ni, tumaini, kwamba Bwana Yesu alitumwa na Mungu; pili, kwamba katika ukamilifu wa kazi yake tumehesabiwa haki; tatu, tunatambua habari zake; nne, tunakuja kumwona mbinguni; tano, tunajifunza kuhusu siri, kitu kikubwa ambacho ni haki yetu kwa sababu ya kuwa mwili wake; sita, kwamba tumeketi pahali pa juu katika Kristo; saba,tumepotelea katika maajabu na katika sifa ndani ya hekima yake mwenyewe.”(J.B.Stoney)

Kwasababu tumekamilika ndani ya Bwana wetu Yesu, haitawezekana kujaribu na kuongeza kwa ile kazi iliyokamilika. Hivi sasa ni swala la kutembea kwa imani na kupokea, kujitwalia, kutoka kwa chemichemi iliyo nyingi zaidi ndani. Walter Marshall anafupisha hapa: “Kufufuka kwa Yesu Kristo kulikuwa ni kufufuka kwetu hadi kwa maisha ya utakatifu,jinsi ilivyo kwa kuanguka kwa Adamu kulikuwa ni kuanguka kwetu

katika kifo cha kiroho: Na sisi si wenyewe waumbaji wa kwanza na waliounda umbile letu jipya lililotakatifu, sio kuliko ufisadi wetu wa kwanza,lakini yote mbili yanaundika tayari kwetu kuyashiriki.

Na kupitia kuungana na Kristo, tunayashiriki yale maisha ya kiroho ambayo yanayashiriki kwa ajili yetu kwa kufufuka kwake, na hapo basi tumewezeshwa kutoa matunda yake; namna andiko linavyoonyesha katika kufananisha kwa kuungana katika ndoa. Warumi7:4 “Kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine,Yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda."

Sehemu yetu si kuzalisha, lakini kukubalika kwa maisha yetu katika Kristo. Hii yafuatia kutafuta ukweli chini ya msingi wa kibibilia: Imani dhahiri ndani yake na kusudi lake kwetu katika Kristo; na tumaini la kuvumilia anapoendelea kupitisha katika kutengenezwa kwa maana ambayo kunahusika. Hakuna yeyote aliyeamini ambaye amepatikana katika kukomaa, hata kama ametimilika katika Kristo. Ukuaji wa kiroho hulazimisha kuweko kwa njaa ya moyo kwa ajili ya Bwana Yesu; Uthabiti, unaotegemea dhamana, kupata kile ambacho ni chetu ndani yake, tukiongezea kutafakari na fikira. Hatutapatikana kamwe katika hekima ya kufanyika kiroho kupitia kwa kuelewa kwa juu juu kwa neno. Tunaweza kutarajia je kuwa na ushirikiano wa kamili na mmoja ambaye tunamjua kidogo?

Ukweli unaofuatia unaweza kuwa fursa ya kufanya zoezi na kuendelea kutafakari huku na fikira. Kinachotakikana ni kutafakari, ndani yake Mungu hukusanya mwenyewe Roho wa kipekee na maisha kama kanuni ya ubinadamu wa kibinafsi kuwa wa kutwaliwa mwenyewe. Katika ufunuo, ambao kwa hakika ni kutafsiri utabiri katika maisha ya kibinafsi
ya mwanadamu, katika kweli, kuunda watu wa Mungu, kubashiri kama huku-yaani, kama maisha kibinafsi-lazima uwekwe katika mwili kwanza katika katikati yako mwenyewe katika ubinadamu. Kwa sababu hii, kadiri ya kitu halisi kipya kinavyohusika, kitu ambacho katika utofauti wake, hakijaonekana bado, kila aina mpya ya maisha, kabla hayajaongezeka yenyewe hadi sehemu nyingi; lazima yaliyomo yawe yamekamilika yakijumuishwa katika umoja uliokamilika, katika kanuni mpya ya kutosha. Na hivyo, kutengeneza mwenyewe kubashiri miongoni mwa watu, kitu cha kwanza kinachohitajika ni kimoja katika zile kanuni ya maisha ya kubashiri yamekuwa ya kibinafsi.

“Ukristo unaweka pamoja ukamilifu wote wa ufunuo katika tabia ya kibinadamu ya Yesu Kristo kama upatanisho wa kitu kipya chenye uhai wa kutabiria, katika ukamilifu wake wa Roho na maisha, ndani na kwa maisha yenyewe ya kibinadamu yenyewe. Kwa mlango wa Kristo ndani ya mtu binafsi, maisha ya kubashiri hugeuka kuwa ya kudumu ndani yetu, sio katika uhusiano wa kidunia wote, lakini kama kanuni ya kibinafsi; ili kwamba mtu hajaumbwa tu na Mungu, lakini kuzaliwa na Mungu. Na mabadiliko ya kukua ya kibinafsi ndani ya namna ya maisha ya Kristo kuna kutimilika katika maendeleo sio ya uadilifu au shirika wa kiutawala, lakini ushirika wa kiasili." (J.T.Beck)

Mbegu huwa katika mwili kamili, utoaji wa maisha hutoka kwake. Hivyo imekamilika, na hakuwezi kuongezeka kamwe. “Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, si

kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika." (1Peti: 23a). "Usipande shamba lako mbegu za namna mbili pamoja."(Law 19: 19). Kunatakiwa kuwa "Si mimi lakini Kristo." Mbegu imekwisha pandwa- sasa swali kwa yule wa ukuaji na kukomaa. Hili tu litaleta matunda ambayo yatadumu. "Maendeleo ya maisha ya kiungu katika Kristo ni kama ukuaji asili katika dunia ya mimea. Haitupasi kuweka jitihada maalum, ni kujiweka tu sisi wenyewe katika hali zinazofaa kwa ukuaji kama huo."

Ni wale tu ambao wamechagua kukua kupitia nguvu na kutofaulu wako katika hali ya kufurahia ukweli kwamba Mungu ni mleta vita katika milki ya maendeleo. "Nguvu zote za Mungu ambazo zimekwisha fuliwa pamoja katika kukamilisha sehemu ya kwanza ya kusudi la milele, kufunuliwa kwa mfano kamili wa Mungu katika mtu Yesu Kristo, yanashughulika sawa ili kukamilisha sehemu ya pili, na kufanya ule mfano katika kila mtoto wa Mungu. "William Law akubali: "Mzizi ambao umeelekezwa kwenye mchanga mwororo, katika tabia bora ya nchi, na kubarikiwa na jua lote lile na hewa na mvua yaweza kuufanyia una uhakika wa kukua bora zaidi, kama vile kila mtu ambaye pengine Roho yake inatamani yale yote ambayo Mungu yuko tayari na kutamani kabisa kumpatia. Kwa maana jua halikutani na tumba linalo tokezea ambalo linajinyoosha kuelekea upande wake na nusu ya hakika kama Mungu, chanzo cha yote mazuri, huwasiliana yeye mwenyewe na nafsi ambayo inatamani kushiriki naye."

Si kwamba maisha yetu yamekamilika tu ndani yake, lakini ushindi wa maana katika mahitaji mengi yote ya maisha hayo. "Wakati unapopigana kupata ushindi, hapo basi umepoteza ushindi mara ya kwanza. Labda adui akushambulie nyumbani kwako au katika biashara yako. Anaifanya hali ambayo hauwezi kukabiliana nayo kwa urahisi. Utafanya nini? Wazo lako la kwanza ni kujitayarisha wewe mwenyewe kwa vita vikubwa na halafu umuombe Mungu akupe ushindi katika vita hivi. Lakini ukifanya hivyo kushinda ni kwa hakika, kwa maana umeacha uwanja ambao ni wako katika Kristo. Kwa shauri ambalo umechukua umeuacha kwa adui. Utafanya nini basi wakati atakapo kuvamia? Unatakiwa tu kutazama juu na kushukuru Bwana. "Bwana nimekumbwa na hali ambayo siwezi kuikabili kwa urahisi. Adui wako shetani ameileta hiyo hali ili kuzunguka kuanguka kwangu, lakini ninakusifu wewe kwa sababu ushindi wako ni ushindi unaohusisha yote. Unafunika hali hii, hali kadhalika. Ninakusifu wewe kwa sababu tayari nina ushindi kamili katika hali hii."

P.S.Usikimbilie- Hawezi: "Msanii kutoka Japan, Hokusai, alisema, 'Toka nikiwa na umri wa miaka sita nilikuwa na moyo wa kupenda sana kuchora maumbo tofauti ya vitu. Wakati nilifika miaka hamsini nilikuwa nimechapisha picha nyingi: Lakini hakuna vile nilitengeneza kabla ya kufikia umri wa miaka sabini kilikuwa cha sifa; Aliaga akiwa na miaka themanini na tisa, akitangaza kuwa kama angepewa miaka mingine mitano angekuwa msanii mashuhuri."

**SURA YA 7**
**KUTWAA**

Hapa kuna somo muhimu ambalo linahusu imani, na mapokezi yake ya kutendwa ambayo tuna uwezo wa kumtumainia Yeye.Kujitwaalia hakumanishi kabisa eti kufaidika kwa kupata kitu kingine kipya, lakini kuwekwa kando kwa kusudi la sisi kuvimiliki kweli vitu ambavyo tayari ni vyetu.

Kukitwaa kitu kwa ajili ya kutembea kwetu katika Kristo, tunageukia kanuni mbili: Kuona kile ambacho ni chetu katika Kristo:na kutambua hitaji letu kwa ajili yake. Katika sehemu hizi mbili kunakaa uwezo wa kujitwalia, kufikia katika kupitia imani thabiti na kupokea kilicho chetu katika Bwana wetu Yesu Kristo.

Kuhusu kanuni ya kwanza, kuona kile ambacho ni chetu, William R.Newell aliandika: “Paulo haulizi kitu ambacho ni cha watakatifu katika sura tatu za kwanza za waefeso lakini kusikiliza tu huku akieneza ukweli mkuu wa ajabu unaofanyika na umilele kuhusu wao; na hadi wakati alikuwa amemaliza kutoa orodha ya ukweli kuhusu wao anawauliza kufanya kitu chochote!

Na wakati yeye hufungua maombi yake kwa mwenendo wao kama watakatifu, kila kitu kinategemea ufunuo uliopeanwa kwanza – ukweli wa tabia zao na mwelekeo kama watakatifu: ‘kwa hiyo nawasihi, mimi niliyemfungua katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili witu wenu mlioitwa (Efe4:1) .Tuepukane na kuwawekea watakatifu orodha ndefu ya ‘masharti’ ya kuingia katika maisha ya baraka ndani ya Kristo; na badala yake, andalizi kwanza la kuwaongoza katika kupitia maisha haya,waonyeshe nafasi yao, matwalio, na tunu katika Kristo tayari wanazo. Kwa hivyo tutafanya kweli na Roho Mtakatifu na hivyo tutakuwa nayo zaidi, na zaidi tunda la kudumu la kazi yetu miongoni mwa watu wa Mungu.”

Wakati tutaona kilicho chetu katika Kristo Yesu, hitaji la kimatendo litatufanya tujitwalie, kupokea jibu kwa hitaji hilo. “Kulikuwa na kutolewa kwa Roho wa Yesu Kristo kwa Paulo, ni hiyo ilifanya kukawa na uwezekano wa Kristo kujitukuza ndani yake. Lilikuwa toleo ambalo kila mara lilikuepo, lakini lilifahamika na kutwaliwa kama na wakati ambapo mitume walikuja kutambua hitaji lake. Maisha yanamaanisha kulete mtawalio wa uvumbuzi wa hitaji letu la Kristo
, na katika kila uvumbuzi wa aina hiyo njia hufunguka kwa kuingia kupya kwa toleo. Haya ni maelezo ambayo ni mengi kiasi kwamba hatuwezi tukaelewa huku kujitumbukiza kwetu ndani ya majaribio mapya ambapo toleo jipya tu la Roho wa Yesu Kristo litakutana na haja yetu. Na jinsi hitaji letu linapopatikana, na jinsi tunavyoonyesha utoshelezi wa Kristo kukutana na hitaji letu la kindani, hivyo pia kutakuwa na kuonyesha kupya kwa utukufu wake kupitia kwetu.” (H.F)

Ukweli unaonekana mara mbili huu wa kuona na kuhitaji unatutoa kutoka kwa mwenendo usionyooka wa kitoto hadi kwa ule wa kuajibika, kutembea ambako ni tofauti kwa imani. Unatuchukua kutoka kwa fikira za “Nisaidie” hadi zile za kutoa shukrani; kutoka kwa kuomba msaada hadi kujitwalia. Tambua lili L.L. Letgers, msaidizi wa mwanzilishi wa watafsiri Bibilia wa Wycliffe, alisema kuhusu haya:

“Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni; katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu. (Efe1:3a.S.V). Ukitazama upesi upesi akilini mwako na upate baraka moja tu ambayo Mungu aweza kutabiri nayo leo, ambayo hajawahi kutubariki nayo, basi aliyomwambia Paulo hayakuwa ya kweli kabisa, kwa sababu alisema, ‘Mungu ame’ Yote yametendwa. ‘Yote yamekwisha’. Mungu ametubariki na baraka zote za kiroho katika ulimwengu wa kiroho! Jinsi C.A. Coate alisema, “Ni kujitwalia ndiko kunatujaribu sisi. Ni mara nyingi kiasi gani tunafika tu kwa kutamani.”

Nyakati zote Roho Mtakatifu atatukumbusha kuhusu hali nyingine ya Neno kupitia njia ya kuchoma, na tutafurahi kuona na kuamini kwamba ni yetu katika Kristo.Yaweza kuwa, kwa mfano, ukweli wa Mathayo 11:28 “Njooni kwangu, nyinyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.” Kando na hali zetu za kawaida, kutokuwa na uhakika, kushindana na wasiwasi ya hali ya dunia inatupa tu yale yanayohitajika kwa mwaamini Adamu, atulie ndani ya Bwana Yesu.Hitaji linalojitokeza, na wakati anapoona utulivu ndani Yake, linalobaki sasa ni kujitwalia.

Kufikia hapo ni uzuri. Aliyeamini huona yale anayoyamiliki katika Kristo, na hitaji linamwezesha kufikia na kutwaa kwa ujasiri na kukubali utulivu unaohitajika. Kujitwalia huku lazima kuwe na uwazi, kulingana na neno, tumaini la kweli. Haitakikani “tuulize vibaya.”Na hapo sasa huja hali ya kupambanua, ambayo ni ufunguo wa yote. Katika namna nyingi za kujitwalia, kuna muda wa kungojea kati kati ya kukubali na kupokea – wingi wa miaka. Wajibu wetu ni kumngojea kwa utulivu wakati wake ukifika wa kufanya kazi katika mwenendo wetu,maisha yetu,ambayo tumeyatwaa katika Kristo – katika hali hii,utulivu wake,uthabiti,uhakika na usalama. “Mungu ----- atendaye mambo kwa ajili ya amngojaye.”(ISA64: 4b,NASB)

T.Austin – Sparks anatupa mawazo mawili yenye thamani kuhusu pengo hili lote la muhimu – kwa kawaida ni mambo ya miaka – kati ya kujitwalia kwenyewe, na hali ya mazoezi tunayopitia. “Kila aina ya ukweli tunaopokea, kama tunapokea kwa upendo, utatupeleka hadi ndani ya mgongano na utaonekana kupitia mgongano. Utakuwa usiostahili hadi wakati kutakuwa na vita juu yake. Chukua nafasi yoyote ambayo Bwana amekuita uchukue, na, iwapo unachukua naye utafanikiwa katika vitu hivyo, na, kutakuwa na kitu cha kuongezea na sababu ya vita. Umechukua nafasi - ndiyo, lakini bado kidogo haujakipata, thamani yake halisi bado haijaonekana. Haujafikia umuhimu wenyewe halisi wa hicho kitu.

Kama matokeo ya kazi yake msalabani, na kamaswala kuu la kufufuka kwake, uzima wa milele umepokelewa tayari na wale ambao wameamini. Lakini huku uzima huo wenyewe ni wa ushindi, usioharibika, usiobomoka, mwamini anatakiwa kuja kwa imani kuujaribu, kuishi kwa huo, kujifunza sheria zake, kubadilisha kwa huo. Kuna akiba ndani ya aliyeamini, ambayo ndani yake haitakikani kuongezwa, kamam vile kulingana na usawa wake.

Kadiri ya ushindi wake, nguvu zake, utukufu wake, mambo yake yawezekanayo kutokea yasiyohusu kitu chochote yaweza kuongezwa juu yake. Lakini chanzo cha hali

tunayopitia ya kiroho, ya maisha ya kiroho,ni kuvumbua,kutwaa, nakuishi kulingana na yale yote maisha huleta na kumaanisha.

Sasa tumeona kitu cha tatu kikihusishwa katika kutwaa kwetu. Baada ya kuona vyote ambavyo tumevimilika katika Kristo, na kutambua hitaji letu, basi ni lazima tumpatie wakati unaotakikana aweze kufanya kule kutwaa ndani ya kutembea kwetu kwa kila siku. Iwapo tunatarajia mahitaji yetu yashughulikiwe katika mahojiano mengine, kitabu kingine cha ibada, mtawalia mwingine maalum wa mikutano, tumaini lingine la “Basi ukweli hautaonekana kamwe.

Katika jambo hili la maendeleo ya Kristo, hakuna njia ya mkato, hakuna njia ya haraka na nyepesi. Mkulima hujenga ndani ya aliyeamini yale ambayo amedhamiria kuhudumia kupitia kwake hadi kwa wengine. Msaada wa uzima kwa wengine, lile mmoja anatenda na kusema lazima itiririke kutoka kwa vile yuko. “Kwa kuwa katika Yeye (Kristo Yesu) ilipendekeza utimilifu wote ukae”; “Ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yenu ipatikanayo na mauti.”(Koli:19;Ebr.3:14;Efe 3:19;Kol 3:3;2Kor.4:11b).

Mara kwa mara tunatamani tu na kuzungumzia juu ya ukweli ambao Roho Mtakatifu hutufunulia katika Neno, kwa maana kusudi lake la kimsingi katika kutupatia sisi  ni kwamba ili tuweze kusimama kwa huo katika imani, tukimngojea kwa ujasiri kuufanya sehemu ya unyoofu wa maisha yetu. “Nabii ni yule ambaye ana historia, yule ambaye ameshughulikiwa na Mungu, Yule ambaye amepitia katika kazi ya kujengwa ya Roho. Wakati mwingine tunaulizwa na wale wanaotarajia kuwa wahubiri kwamba ni siku ngapi zitachukuliwa kuandaa ujumbe wa kufunza. Jibu ni: Kwa miaka kumi, na labda karibu na ishirini! Kwa mhubiri mambo kwa Mungu ni kulingana na kitu kinachohubiriwa. Mungu huchagua kama manabii wake wale ambao tayari amewatengenezea kile anachotaka kukitumia kama ujumbe wake kwa siku ya lea.”

## SURA YA 8
## KUTHIBITISHWA

Jinsi fikira zetu zinavyosonga kutoka badiliko la ukweli wa kuzaliwa, mpaka ukweli wa uthibitisho, kutafaa kuzingatia kwa ufupi ni nini viongozi, wenye heshima ya Mungu kupitia miaka, wanaweza kusema kuhusu uthibitisho, namna umekuwa mkuu katika Warumi 6.

Evan H. Hopkins: “Taabu ya aliyeamini ambaye anajua Kristo kama mwenye haki yake si dhambi kama kwa makosa yake, lakini dhambi kama kwa nguvu zake zinazotawala. Kwa maneno mengine si kutoka kwa dhambi kama uzito, au kosa, ambako anatafuta kujiweka huru – kwa kuwa anaona kwamba Mungu amemjulisha kamili kutoka kwa shtaka na adhabu ya dhambi – lakini ni kutoka katika dhambi kama Bwana. Kujua njia ya Mungu ya ukombozi kutoka kwa dhambi kama Bwana lazima akamate ukweli ulioko katika sura sita ya Warumi. Hapo tutaona kile Mungu ametenda, sio na dhambi zetu – swali lile ambalo mtume ameshughulikia katika sura zilizotangulia mbele – lakini na sisi wenyewe, watendaji na watumwa wa dhambi. Ameweka mtu wa zamani – sisi wa asili – mahali ambapo aliweka dhambi zetu, kwa kutaja, msalabani na Kristo. “Mkijua ya kuwa mtu wetu wa kale alisulubishwa pamoja naye.”(Rum6: 6). Mwamini hapo huona sio tu kwamba Kristo alikufa kwa ajili yake – badalaya – lakini kwamba alikufa na Kristo – Thibitisho.”(Wazo juu ya uzima na uzuri, P.50)

Andrew Murray: “Kama Kristo, mwamini pia amekufa kwa dhambi; yeye ndiye ana Yesu, kwa mfano wa kifo chake (Rum6: 5). Na kama hekima ile Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi kama upatanisho wetu ni kanuni kwa kuhesabiwa haki kwetu kwa hivyo hekima ambayo Kristo na sisi pamoja naye katika mfano wa kifo chake, tumekufa kwa dhambi, ni kuhesabiwa haki kwetu kwa lazima.”(Kama Kristo, P.176).

J.Hudson Taylor: “Kwa sababu Kristo Ameishi hivyo ndani ya moyo wangu kwa imani, nimekuwa na furaha iliyoje! Na sasa Kristo Yu aishi ndani yangu, na maisha ninayoyaishi sasa katika mwili ninaishi kupitia kwa imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, na akajipeana Yeye mwenyewe kwa ajili yangu tusiangalie kwa hali hii, ukweli huu, kama kwa ambao ni wachache. Ni haki za kuzaliwa kwa kila mtoto wa Mungu, na hakuna yeyote awezaye kujigawanyisha nao bila ya kutomtiii Bwana.”(Siri ya kiroho, P.116).

William R. Newell: “Kwa wale ambao hukataa au huacha kujihesabu wenyewe wafu katika vile Mungu anavyoagiza, tunalete swali. Utawezaje kuamini kwamba Kristo kwa kweli alifunua makosa ya dhambi zako na kwamba hautakutana nazo katika siku ile ya hukumu? Ni Neno la Mungu tu ambalo hukueleza kwamba Kristo alitoa dhambi zako katika mwili wake mwenyewe pale msalabani. Na ni hilo Neno ambalo hukueleza kwamba wewe jinsi ulivyounganisha Adamu, ulikufa na Kristo, yule mtu wako wa kale alisulubishwa, kwamba kwa vile uko katika Kristo ulishiriki kifo chake katika dhambi, na kwa hivyo yakupasa kuhesabu ushirikiano wako wa sasa na dhambi katika Kristo ndani ya Mungu.”(Warumi, msitari kwa msitari, uk 227).

Lewis Sperry Chafer: “Maudhui chini ya kukumbushwa yalihusu kifo cha Kristo kama vile kifo hicho kilihusiana na hukumu ya kiungu cha dhambi cha asili katika mtoto wa Mungu. Lazima katika hukumu kama huo na ufunuo wa hali ya juu kwamba hukumu hizi sasa zimekamilika ndani yetu zimefunuliwa katika Warumi 6:1-10. Ujumbe huu ni msingi na tena ni ufunguo kwa uwezekano wa ‘safari katika Roho’ (Yeye Yule Aliye wa kiroho, uk154).

R.Paxson: “Yule ‘mimi’ wa zamani ndani Yake na mimi alisulubishwa kwa hukumu na Kristo ‘Mlikufa’ na kifo chenu kinaanzia wakati wa kifo cha Kristo. ‘Mtu wa zamani’, ‘Mwenyewe’ wa zamani katika idadi ya Mungu ilichukuliwa hadi msalabani pamoja na Kristo na kusulubishwa na kupelekwa kaburini na Kristo na kuzikwa. Hakikisho la ukombozi kutoka kwa eneo la ‘mwili’ na kutolewa kwa ‘Mtu wa kale’ hutulia kwa kushika na kukubali ukweli huu wa kusaidia katika kusulubishwa”(Uzima wa ndege juu, Vol –2,pp.78, 79.)

Watchman Nee: ‘Dhambi zetu zilishughulikiwa na damu, sisi wenyewe tunashughulikiwa na msalaba. Damu hutengeneza msamaha wetu, msalaba huleta ukombozi kutoka kwa kile ambacho tuko ndani ya Adamu. Damu inaweza kusafisha dhambi zangu, lakini haiwezi kuosha mimi wa zamani: Nahitaji msalaba kusulubisha mimi – mwenye dhambi.” (Maisha ya kawaida ya mkristo, uk.25)

L.E.Maxwell:”Waamini katika Kristo waliunganishwa kwake pale msalabani, walikuwa na umoja na yeye katika kifo na kufufuka. Tulikufa na Kristo. Alikufa kwa ajili yetu, na tulikufa naye Huu ni ukweli mkuu, ukweli wa waamini wote”(Ushindi wa mkristo, uk 11

Norman. B. Harrison: “Hii ni alama dhahiri ya mkristo hali ya msalaba. Sio tu kwamba Kristo alikufa kwa ajili yetu, lakini kwamba tulikufa naye. ‘Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye’(Rum 55” (Upande wake dhidi ya upande wetu,uk.40).

F.J.Huegel: “Ikiwa Luther mkuu, na ujumbe wake wa kusisimua wa kuhesabiwa wa wenye dhambi wa sasa waliohesabiwa haki pamoja na Bwana aliyesulubishwa, si mprotestanti aliyezuiliwa atakuwa juu zaidi siku hizi? Hauwezi kuwa huru kutokana na nyama yenye vidonda? “(Msalaba wa Kristo, uk.84).

Alexander R.Hay: “Mwamini amejumuishwa na Kristo katika kifo chake. Katika umoja huu na Kristo, nyama, ‘Mwili wa dhambi – wote ulianguka, kubomolewa na dhambi kuwa na werevu wake, nia na tamaa – unahukumiwa na kusulubishwa. Kwa imani, aliyeamini huhesabu yeye mwenyewe ‘Mtu katika dhambi.”(Warumi 6:3-14)” (N.T.Mpango kwa kanisa & Misionari. P.310).

T.Austin –Sparks: “Sehemu ya hali yetu ya kiroho yaweza kuwa kuu na furaha inayofurika, na hisia ya uhuru ya ajabu. Katika sura hii vitu vilivyopotea husemwa mara nyingi kama ukombozi wote wa ujumla na ushindi wa mwisho. Halafu kwa weza kukawa, na kawaida huwa, huja namna ambayo kuhukumika ni swala kuu. Yaweza kuwa sana hali ya Warumi 7.Hii itasababisha, chini ya mkono wa Bwana, hekima kamili ya maana ya uthibitisho na Kristo, kama katika Warumi 6 furaha mtu yule ambaye ameshauriwa katika haya tangu mwanzo.” (Mtu ni nini? Uk. 61). J.Penn – Lewis: “Ikiwa tofauti kati ya “Kristo kufa kwa ajili yetu” na ‘kufa kwetu naye,’

haijatambuliwa, kujulikana, na kuwekwa katika matendo, yaweza kuthibitishwa kwa usalama kwamba ubinafsi ndio bado umetawala katika maisha.” (Ukumbuko, uk.26)

William Culbertson: “Nani alikufa msalabani; lakini nani tena alifia pale? Kujua hili kuwa mtu wetu wa kale alisulubishwa naye kwamba mwili wa dhambi waweza kuharibiwa, kwamba tangu sasa haitupasi kutumikia dhambi. Sasa iwapo tumekufa na Kristo, tunaamini kwamba tutaishi tena pamoja naye:(Rum 6:6-8)"”Maandalizi ya Mungu kwa kuishi kutakatifu, uk.46)”

Reginald Wallis: “Mungu asema katika mwisho, ‘Mtoto wangu, jinsi ulivyohesabu kazi nyingine ya Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu wako, basi sasa nenda hatua nyingine mbele na uhesabu kazi yake wakilishi kwa ajili ya ushindi wako siku baada ya siku. Unaamini Bwana Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako kwa sababu Mungu alisema hivyo. Sasa chukua hatua nyingine. Kubali kwa imani ukweli zaidi kwamba ulikufa naye; k.m. kwamba ‘Utu wako wa zamani ulisulubishwa naye. “(Maisha yangu mapya, uk.51)

James R.McConkey: “Kwa sababu alikufa ‘kifo hakimtawali tena’, na kwa sababu ya umoja wetu naye ‘Dhambi haitawatawala,’ hata kama imo ndani yenu. ‘kudhania kwetu’sisi wenyewe tumekufa kwa dhambi katika Yesu Kristo hakuifanyi kuwa ukweli – tayari ni ukweli kupitia kwa umoja wetu naye. Kudhania kwetu kuwa hiyo ni kweli tu kunatufanya sisi kuanza kutambua ukweli katika hali tunayopitia.”(Njia ya ushindi uk.16).

## SURA YA 9
## UWAKFU

Yaweza ikawa vyema kusisitiza vidokezo vingi hapa tu

1. Mwamini kamwe hakuwekwa katika ukomavu ambao ni safi na wakiroho kupitia kwa mikutano ya kushurutishwa, na ushauri wa mara kwa mara, wala sio kabla ya yeye kuandaliwa na Roho.
2. Maendeleo mazuri ni kwa msingi wa kufahamu, kuelewa, na kutwaa ukweli katika Kristo ambao unafanya ukuaji wa halali.
3. Namna ya mambo tunayopitia ya ukweli wote, na haswa yale tunayoyaita ukweli wa kindani, umefunikwa kwa yote lakini kwa moyo wenye hitaji. Hadi mmoja atakapotambua hitaji lake la kuendelea kiroho, hatawahi kamwe kufikia zaidi ya ukweli wa kuzaliwa – mtoto halisi katika Kristo. “Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu;”(HEB 6:1, kwa upana).

Somo hili la wakfu laonekana kama linaloeleweka vibaya na waamini wengi. Wengi, haswa wale waliowachanga katika Kristo Bwana, watolewa vitisho vya mara kwa mara katika swala hili la kujipeana,au kujipa sharti. Fimbo ambayo kwa wakati mwingi hutumika ni: “Bwana Yesu alipeana yote yake kwa ajili yako, na sasa machache yale waweza kufanya ni upeane yako yote kwa ajili yake!
Mwamini anashauriwa na kushirikishwa kuwekwa wakfu, kujitoa, kuweka maisha yake kwa Kristo kwa msingi wa mapenzi yake na shukrani kwa yale ambayo yametendeka kwa niaba yake pale Kalvari.

Ni mara ngapi jamii ya wastani ya wale wanaoabudu imewekwa kupitia kwenye utaratibu huu. Ni mara ngapi ya mwamini wa kipekee ameshawishiwa hadi kuwekwa wakfu na zaidi, hujiachilia na tena zaidi, kujipa sharti na zaidi mwenyewe kwa Kristo! Mbona sasa kwa kitambo kidogo yule aliyeamini hugeuka na kuogopa mikutano na ujumbe kama huu? Sawa, kuna sababu kadha wa kadha za mateso, kugaagaa, na kutofaulu; na Bwana asifiwe, kuna majibu ya maandiko ambayo yanapatikana kwa wale wote wanaohitaji na wanoyataka.

Kwanza, ni ubatili mtupu kumtarajia yule aliyeamini, kwa njia ya kuwekwa wakfu, kujipeana, aukujipa sharti, kupiga hatua kutoka kwa eneo lake la badala (Rum 3-5), hadi kwa ukweli ule wa kindani katika Warumi 8 na 12:1 Kuna eneo la pande zote muhimu la kweli unaothibitisha katika Warumi 6 na 7 ambao hauwezi kuachwa. Kila mkristo mwenye moyo wenye njaa anatamani kuwekwa wakfu kamili na kutengenezwa kwa ajili ya maisha na huduma ya kufaa. Na kutoka mwanzo, mpaka hali ngumu tunayopitia humfunza njia nyingine, mwamini anayemaanisha vema hufikiria kuwa kwa maana ana nia ya kumtii Mungu na kuwa jinsi anavyotarajia yeyey awe, anapaswa kujaribu kuiendeleza kupitia kwa jitihada za kujiweka wakfu za kibinafsi kwa msaada

wake. Yeye hutafuta kupambana kupitia hisia za upendo, km;Yeye alinifanyia, kwa hivyo ni lazima nimfanyie.

Mawazo mawili yafuatayo ya Andrew Murray yatasaidia hapa. “Kutambuliwa kwa haraka na mipango ya Mungu husababisha maoni kwamba huku sababu ya haki ni kazi ya Mungu, kwa njia ya imani katika Kristo, (Kukua) katika utakaso ni kazi yetu, itakayofanyika chini ya shirikisho la shukrani tunayohisi kwa ukombozi ambao tumepitia, na kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Lakini mkristo mwenye bidii hatimaye hupata jinsi shukrani ndogo yaweza kusambaza nguvu. Wakati anapofikiri kwamba kuomba kwingi kutaeneza, yeye hakutakuwa, lakini kama maombi yalivyo, haijatosha. Kwa mara nyingi mwamini hupambana bila kuwa na tumaini kwa miaka mingi, hadi atakaposikiliza mafundisho ya Roho Mtakatifu, huku akimtukuza Kristo tena, nakumfunua Kristo, ambaye ni utakazo wetu, na kutwaliwa na amani pekee yake.

“Mungu hufanya kwa nia ya yuko tayari kutekeleza kazi kwa kufanya (Fil.2:13), lakini, tazama wakristo wengi hawaelewi hili. Wao hufikiri kwa kuwa wana nia hilo latosha, na kwamba sasa wanaweza kufanya . Hivyo si kweli. Nia mpya ni kipawa cha kudumu, hesabu ya asili mpya. Nguvu za kutenda si kipawa cha kudumu, lakini kila wakati lazima kipokelewe kutoka kwa Roho Mtakatifu. Ni binadamu ambaye anafahamu kuhusu umuhimu wake mwenyewe kama vile mwamini ambaye atajifunza kwamba kupitia Roho Mtakatifu anaweza kuwa na maisha matakatifu.” Pengine mmoja huitwa akazungumzie kuhusu ubaya wa kitu ambacho ni kizuri, ili uwasilishe uzuri wake. Hisia za upendo kutoka kwazo kuishi maisha ya ukristo na kumtumikia Bwana ni vyema, ni ya heshima, lakini haitoshi – haswa kwa sababu hii si motisha iliyokubalika naye.

Kama wakristo wanaendelea kukua, ni wakati wetu mzuri kuona umuhimu wa kwenda zaidi ya madhumuni ya upendo hadi madhumuni ya maisha. “Kwa maana kuishi kwangu ni Kristo.”(Fil.1:21a). Kuwekwa
Wakfu kwetu, kujipeana au kuahidi  hakutainua kamwe kama ni kuitika kwetu kwake kutoka kwa mvuto mwingine wowote ule kuliko kuitikia kwa maisha yake ndani yetu Kujitoa kwetu kwake kwa msingi mwingine tofauti kutasababisha tu kujaribu kwetu kuishi kwa Kristo katika maisha ya binafsi. Na hata kama kulikuwa kuna uwezekano, hangeweza kuyakubali, kwa sababu katika milki hiyo hakuishi kitu chochote kizuri (Rum7:18;Maisha ya kale pale msalabani na kuyasulubisha (Rum 6:6 ,Gal 2:20; 2Tim.2:11;1Pita.2:24)

J.C.Metcalfe anaona shida na suluhisho: “Mafundisho ya kisa ya kuwekwa, kwa ‘utu wa zamani; unaojaribu kuepuka hukumu ya kifo na hatimaye, husababisha tu mateso na kushindwa. Wakati, walakini, wewe na mimi tumejiandaa, Katika uvumilivu kiasi, kufanya ukweli wa kifo chetu na Kristo msingi wetu wa kila siku na mtiririko wa maisha mapya, na kukutana na haja ya nyoyo zenye kiu inayotuzunguka.”

Hapa kuna shida ya mambo. Swali ni hili, Ni maisha yapi ambayo yapaswa kuwekwa wakfu kwake?, maisha yetu wenyewe ya kale,au maisha mapya ya ukristo? Mungu hawezi kamwe kukubali chochote kutoka kwa ya kale – Yeye huona na kutambua yale tu yanayompendeza mwanawe, ambaye ni maisha yetu. Kwa hivyo Mungu analo tu sharti moja la kuwekwa wakfu: “Mjitolee nyingi wenyewe kwa Mungu,

kama wale walio hai kutoka kwa wafu.”(Rum 6:13). Hili ndilo eneo letu tu, na kutoka katika jukwaa hili tujihesabu sisi wenyewe wafu katika dhambi, utu, sheria, dunia, na waliohai kwa Mungu katika Kristo aliyefufuka – kutembea katika “Upya wa maisha,” “Maisha yaliyoinuka.”(Rum6: 11,4b)

“Jitoeni nyingi wenyewe kwa Mungu kama wale walio hai kutoka kwa wafu.”(Rum 6:13, Nasb). Hapo ndipo pahali pa kuwekwa wakfu. Kwa waamini ‘Kujiweka wakfu wenyewe kwa Mungu kuliko kujifunza umoja wao na Kristo katika kifo na kufufuka (thibitisho) ni kujipeana tu kwa Mungu sehemu za mtu asili, ambazo hawezi akakubali. Ni wale tu ambao wako hai kutoka kwa wafu – maana yake, ambao wametwaliwa vikamilifu kwa kufunua naye katika kifo – wamekaribishwa kutoa washirika wao kama vyombo kwa Mungu.”

“Mungu atuuliza kutoa miili yetu kama dhabihu iliyo hai kwake (Rum 2:1). Hadi tutakapofanya hivyo, hapana lingine lolote twaweza kulitenda.Jua usia huu unatoka kwa Warumi 6. Kuna sababu ya mipangilio huu – kusulubishwa huja kabla ya kuwekwa wakfu. Hii ndiyo sababu ya watu wengi wenye uwaminifu hutembea chini ya upande mmoja wa marefu ya kanisa tena na tena, waliwekwa wakfu nafasi zile ambazo hazijasulubishwa kwa Mungu.”(H.Duncan). Hii ndiyo sababu ya ukweli wa uthibitisho lazima uwasilishwe kwa uangalifu na makini, kueleweka kwanza, na ukweli wao kuingiliwa. Hatuwezi kwenda hata umbali wa kuwekwa wakfu bila wao! Wengi huhisi kwamba uthibitisho ni  “Usisitizi” somo la kusisimua linalohudumiwa katika mazungumzo chache ya maisha ya kindani na. Lakini ukweli huu si mzingo; ni wa kimsingi. “Sura ya sita ya Warumi sio swala la ukweli, lakini ukweli wa kimsingi ambao kwake kila aliyeamini lazima asimame juu yake kujua chochote kuhusu ushindi.”

“Ukweli wote wa (kuthibitisha) tumejifunza kuhusu msalaba, wa kifo chetu na Kristo, kifo chetu katika dhambi naye, kubadilika kwetu hadi kifoni kama vile punje ya ngano inavyoanguka chini ife, ni maandalizi kwa ajili ya maisha ya ushindi. Ni msingi wa muhimu kwa hayo.”

“Mafunzo ya uangalifu ya barua zote za Paulo yameonyesha kwamba yameandikwa kwa msingi wa msalaba ambao umewekwa mbele katika Warumi 6 – Ukweli kwamba Mungu hutoa maisha ya kale ya Adamu yaliyoanguka kwa msalaba, na hana lolote la kusema kwayo. Mungu hushughulikia waamini wote kwa msingi – ‘Katika Kristo ulikufa! Lakini kanisa la Kristo, lote hupuuza ukweli huu. Huchukulia viumbe vilivyoanguka (Maisha ya kibinafsi) kama yale yanayoweza kuimarika, na maana ya msalaba kuua kabila la Adamu kama lililoharibika kiasi cha kutoweza kukarabatiwa, hivi limebatilishwa.”

## SURA YA I0
## NAFSI

Mojawapo ya vipengele muhimu katika ukuaji wa kikristo ni ufunuo wa maisha ya kibinafsi na Roho Mtakatifu kwa mwamini. Nafsi ni ya kimwili, maisha ya tamaa ya kimwili ya asili, maisha ya Adamu wa kwanza- “Wafu katika makosa na dhambi.”(Efe.2:1): Waliochafuka mbele ya Mungu (Gal.5:19-21); maisha ambayo ndani yake hamna chochcote kizuri usoni mwa Mungu (Rum 7:18). Hapana pengine katika kanuni za kiroho ambapo panamaanisha kuliko hapa. Plato, na yake “Jua wewe mwenyewe,”alikuwa sawa zaidi kuliko alivyojua lakini bado nusu sawa tu. Paulo na ya Mungu “Si mimi bali Kristo,”alikuwa sawa kabisa!

Ili mmoja aweze kuenda zaidi ya kujua tu kuhusu Bwana Yesu,na kuingia katika hekima ya kibinafsi ya kudumu na kukuwa na kushiriki naye,mtu lazima kwanza ajijue mwenyewe. Kujifikiria mwenyewe hakuhusiki hapa – Roho Mtakatifu hutumia ufunuo wa kujaribu. Kwanza, mwamini hujifunza “Si mimi,”halafu “Bali Kristo” kwanza, punje ya ngano isipoanguka chini na kufa, huishi pekee yake,”halafu”lakini iwapo itakufa huzaa matunda mengi.”(Yon.12: 24). Kwanza, “Daima kupeanwa kwa kifo,” halafu “Kwamba maisha tena ya Kristo yanaweza yakaonekana.”(2Kor.4: 11). Katika huduma: kwanza, “Kifo hufanya ndani yetu,” halafu. “lakini uzima ndani yako.”(2Kor.4: 12). Uzima na kufufuka wote hutoka kwenye kifo, pengine haungekuwa uzima wa kufufuka – Uzima wake wa kupanda (Rum.6:5,6).Yafaa tutoe mazao sisi wenyewe kwa Mungu kama wale ambao wako hai kutoka kwa wafu (Rum.6:13).

Kwa miaka kadhaa sasa mazingira ya uinjilisti yamechukuliwa sana na mageuzi yaitwayo “kujitolea” ambayo daima, yahuzunisha kusema, huleta machache kuliko ukosefu wa kiroho wakati kuna mfano wa maisha huchanua kwa usiku mmoja kuwa maua kamili; na hatimaye hugeuka kuwa nzito na matunda ya “Mabadiliko,” “Angavu,” nafsi ambayo imeunganishwa na kazi nyingi, huduma ya haraka haraka. Tokea ubaya wa kitu hiki ni kwamba nafsi iko nyumbani na hukaa katika kumetameta kwake kwote, na ni nadra sana kupatikana jinsi haswa ilivyo. Yote ni  “Nyoyo na mawaa”yasiyo na tofauti.

Kuzaliwa kupya kwenye afya, ambako kuko kwenye msingi wa thibitisho la dhambi, na kutubu kwa Mungu, huanza wazi na kuwa na nguvu na upendo wa kujitolea kwa mwokozi. Lakini kabla ya kitambo kidogo, hapo huja kutambua kwa kuzamisha kwa ulimwengu ambao ndani mwake humburuta mmoja nyuma hadi kwa kujipenda, kwa ulimwengu, kwa mamlaka ya sheria, kwa dhambi. Kujifunza huku kwa hala ya kuvunja moyo kwa hali ya dhambi kabisa na nguvu za kutawala za kibinafsi katika maisha ya kila siku ya ukristo, ndiyo njia ambayo tunakuja kumtambua Bwana Yesu zaidi ya sehemu ya kuzaliwa – kama mwokozi wetu; Kwa sehemu ya ukuaji – kama Bwana wetu na uzima. “Kwangu kuishi ni Kristo.”Hakuna mwamini yeyote

ambaye kwa Ukweli atamjua Bwana Yesu kama uzima wake hadi atakapokujua hali anayopitia maisha ni hatari ya kibinafsi ya kina ndani yake namna yalivyo.

Katika mikutano ya maisha ya kiroho miaka mingi iliyopita, Daktari C.I.Scofield alisema, “Si kila mtu kwa njia yoyote ile, amepitia hali ya Warumi saba, ule uchungu wa migongano, ya shauku ya kufanya yale hawezi kuyafanya, ya kuwa na hamu ya kufanya mema tunapata hatuwezi kufanya. Ni baraka kuu wakati mtu anapoingia katika Warumi saba na kuanza kutambua mgongano wa ajabu wa mvutano wake na kushindwa: Kwasababu hatua ya kwanza ya kutoka katika mvutano huo wa sura ya nane, ni kuingia katika ile ya saba. Kwa madarasa yote ya watu wenye mahitaji, lile lenye hitaji kuliko mengine duniani si lile ambalo lina huzuni sana, lakini yale ambayo hayaujui, na yale ambayo yametosheka na kuamka katika karibu maandamano yote ya kusikitisha yasiyokuwepo ambayo ni yao katika Kristo.”

J.C.Metcalfe anaupa ukweli huu ushaidi wa kuongezea: “Yule miongoni mwa wengi, Mkristo mchanga, ambaye hajatahadharishwa kuhusu safari hii ya lazima ya uvumbuzi ambayo kwake Roho Mtakatifu kwa hakika atamwanzishia (Rum7) , Ametumbukizwa katika kukata tamaa ambako hakuwezi kutibika kwa mtazamo wa kidhambi ambao ni wake kiasili. Katika mara ya kwanza amefurahia sana katika msamaha wa dhambi zake, na kukubalika kwake na Mungu; lakini baada ya muda mfupi alianza kutambua kwamba yote si sawa, na kwamba hajafaulu na kuanguka kutoka kiwango cha juu ambacho alijiwekea kufika katika hali ya kwanza ya kugeuka kwake

Anaanza kujua kitu kuhusu hali ambayo Paulo ameieleza: “Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo, ninalolitenda (Rum7:15) na, katika tokeo,anahisi kwamba msingi umeanguka kutoka kwa maisha yake ya ukristo:na pengine adui anamnong’onezea kwamba si vizuri katika kuendelea kwake, kwa sababu hataweza kamwe kutengeneza cheo. Anatambua kwa ufupi namna hali yake ya kiafya ilivyo, na kwamba uvumbuzi huu uliodhoofika ni mwanzo kwa mlolongo bora wa uvumbuzi zaidi wa vitu ambavyo Mungu ameviunda kwa utajiri wake wa milele. Katika maisha Mungu anatuonyesha makosa yetu na hitaji, kabla hajakuwa na uwezo wa kutuongoza katika milki ya neema, ambayo ndani yake tutauona utukufu wake.”

Ufunuo wa kibinafsi huendeleza ufunuo wa kiungu – hiyo ni kanuni ya kuzaliwa kiroho. Mwamini ambaye anakumbana na mvutano na kutofaulu ni mkristo ambaye anashughulikiwa na Bwana kwa uangalifu na kwa upendo katika njia ya kibinafsi. Anapitishwa katika hali (kiasi cha miaka) ya ufunuo wa kibinafsi na katika kifo, msingi wa kipekee ambao kwa huo “Kujua Yeye, na uwezo wa kufufuka kwake,na ushirika wa mateso yake nikifananishwa na kufa kwake.”(Fil:3:10).

Mungu hufanya kwa njia ya fumbo ya maneno. Mafanikio huja kwa njia ya kutofaulu; maisha hutoka kwa kifo, n.k.swala la pekee katika maisha ya mwamini ambalo linavuruga ni lile ambalo huenda kwa namna yoyote – maisha mapya hayatadhurika au kuathiriwa. Mgawanyiko huu ni kitu ambacho mwamini hawezi kuingia ndani yake wala kubuni kwa yeye mwenyewe – nafsi haitaitupilia nje nafsi. Ataongoza hadi ndani yake kwa rehema za Roho Mtakatifu – hadi kutofaulu: hafifu na

jumla. “Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti.”(2Kor.4:11).Kwa mara nyingi njia ambazo  hutumiwa na Roho ni ile ya kutookolewa na mwenzio, au hata aliyeokolewa! Au afya iliyodhoofika, ndio, na afya nzuri, pia! Vitu elfu moja na moja vyatumiwa naye – haswa, kila kitu (Rum 8:28,29), kuleta nje mabaya kutoka kwetu, kwanza kutuwezesha sisi kuona kwamba maisha ya Kristo lazima yawe “Si mimi, bali Kristo.”Watu, hali za kawaida, n.k;havileti kutofaulu. Mapokeo ya nafsi kwa hivi vitu ndiyo yanayosababisha, na shida moja ambayo yapaswa kushughulikiwa. “Ni mimi, ni mimi, Bwana.”

Wengi wetu hatimaye wamejua vile kulikuwa kufurahi katika neema ya Mungu bila kufahamu kabisa tabia halisi ya mwili. Imegunduliwa mara nyingi kwamba mahali kuna kustawi kwa hali ya juu kwa furaha katika mwongofu mchanga, kuna purukushani daima ambayo hushindwa kutambua kwamba mwili haubadiliki katika hali hiyo neema ya Mungu huchukuliwi katika njia ya kujitegemea nafsi; kuna kutojiamini kidogo sana, au hisia ya unyonge na kujitegemea. Na matokeo ya lazima ni kuanguka, au mfatano wa kuanguka, hiyo polepole hurejesha nyumbani dhamira za waamini unyonge wao na ukosefu wa akili jinsi ilivyo kwenye mwili.”(C.A.Coates).

Evans Hopkins anashirikisha mwanga mkubwa katika somo letu: “Jinsi gani miundo ambayo haina mwisho ambayo nafsi huonekana. Wengine wamejawa na nafsi nzuri. Wanajifurahisha wenyewe katika utukufu wao. Wengine wametwaaliwa zaidi na nafsi mbaya. Milele wanaugua kwa ajili ya upungufu wao, na kukazana na mwili kana kwamba walidhania katika muda kuubadilisha. Ni lini tushawishikeeti ni vibaya kabisa kwamba ni mambo yasiyoweza kupatikana tena? Hali zetu tunazopitia, juu, katika nguvu za Mungu, ni sawa na hali zetu, hini, katika kukoma kutoka kwa nafsi.

“Ni kweli, kujihesabu mwenyewe kuwa dhaifu katika kurejelea dhambi? La, chini zaidi ya hapo. Ni kweli, ujihesabu wewe kuwa anayeangamia? La, chini bado. “Jihesabu wewe mwenyewe kuwa mfu.”- (Rum 6:11)-Hakika katika dhambi! Wengine huamini kwamba wao ni wanyonge. Lakini hilo lamaanisha nini? Kwamba wana nguvu. Lakini mtu anapokufa hana nguvu. Lazima twenende wa kweli kwamba tumekufa kwa kulingana na dhambi. Hatutaongea tena juu ya shida kama kupinga majaribu kulingana na sisi wenyewe. Tutachukua sehemu ya chini kabisa, na kusema kwamba lisilowezekana kwa nafsi lawezekana kwa MunguTutachukuwa nafasi zetu upande wa kufufuka wa msalaba, na katika kufanya hayo tunaacha nyuma maisha ya nafsi ya zamani hadi maisha mapya ya Kristo. Kuishi ndani yake ambaye ni maisha yetu,ni kuwa katika nguvu za Mungu.”Mtu mmoja anasema vema kwamba “Kuna wengi ‘waliotengwa na dunia’ wakristo ambao hawajajitenga wenyewe ‘wakristo.’

## SURA YA 11
## KUJIKANA

Wakati mwamini anapoanza kugundua udhalimu wa ajabu wa maisha ya kibinafsi, au amekazana bila kukoma dhidi ya udhalimu huo, hujihushisha sana kujikana na uhuru unaojitokeza wa kutulia na kukua katika Kristo. Mwanadamu ana njia nyingi za kutafuta kuhepa utumwa wa nafasi; Mungu ana njia moja tu kwanza, baadhi ya njia hizi ambazo mwanadamu ameweka fikra kwazo

KUOZA:
Kujikana wewe mwenyewe huhakikisha vitu kwa muda, au hata wakati wote, hakukaribii hata na jibu kwa sababu asili ya kale itarekebika na kustawi chini ya hali zozote – chochote kilichopungukiwa na kifo hadi nafsi. “Kumekuwa na wale ambao wamefikiria kwamba kujiondoa kwao wenyewe nje ya njia ilikuwa ni lazima kujiondoa kutoka katika jamii: Kwa hivyo walikataa ushirikiano wote wa kibinadamu wa asili na kuenda hadi jangwani au katika korokoro ya mpweke kufunga na kufanya kazi na bidii ili kuozesha mwili. Huku fikra zao zilikuwa nzuri ni vigumu kueleza kuhusu njia zao wanazotumia. Kwa kuwa si kibibilia kuamini kwamba asili ya yule Adamu wa kale anaweza kutawaliwa kwa njia hiyo. Haizalishi chochote kidogo kuliko kifo cha msalaba .Kwa ujumla ni vigumu mno kuuliwa kwa kutumia mwili vibaya au kuua upendo.”(A.W.Tozer).

USHINDI:
Kwa hakika mambo yaliyoandikwa haswa na nguvu za kumaliza yote ni bidii ya mwamini kushinda na kuongoza hii nafasi kuasi. Mikutano, zaidi, mafundisho ya bibilia zaidi, maombi zaidi yote yamerudiwa mara kwa mara, lakini hayo si majibu ya Mungu kwa shida hii.

MAFUNDISHO:
Hapa kuna la kupendeza ambalo limejaribiwa na kupatikana kuwa haba kupitia miaka mingi. Mafundisho mazuri ya Ukristo na tamaduni nyumbani kuzuri, makanisani, na shuleni yametegemea kwa kutuliza ile asili ya kale na kuilainisha.

UFUFUO:
Kutofaulu kwingine kumekuwa kule Kwa kufanya mikutanao maalum mara moja au mbili kwa mwaka. Hii inahusisha uongozi wa nje (mgeni kwa shida za kibinafsi), na masharti ya uamsho wa kuharibu (kukiri, maafikiano mapya n.k), katika tumaini kwamba kitu kitabadilika – lakini ni nadra sana kufanyika, na si kwa muda mrefu.

UKUAJI:
Wakristo wengi wapendwa huendelea tu kufanya kazi kwa bidii (au mbioni) kupitia kwa utaratibu wa kuangamiza wa matekelezo yao mengi ya kanisa na zamu, wakitarajia

kwamba kwa wakati nafsi itabadilika kwa ubora vile wanavyoendelea kukua. Lakini nafsi haitabadilika kamwe kuwa kitu kingine lakini zaidi kama sawa! “Kile kilichozaliwa kwa mwili ni mwili.”(Yn 6:6a). Kwa wakati mwingine nafsi hii ni mbaya kwa ujumla kama vile wakati imekasirika, yenye chuki, si karimu, dhalimu, sio na kweli, sio na upendo, choyo. Katika hali nyingine kuonekana kwa nje kuzuri husetiri moyo uliojaa uovu, kama vile tunavyojivunia mateso yetu, kujivunia juu ya huduma yetu ya ukristo, tukijawa na maringo ya imani yetu halisi. Na hali ya kuwa mbele zaidi na kujivunia Kwa kawaida kwa mlio wa sauti ya mmoja huharibu mikutano mingi ya maombi.”

KUTAKASIKA:

Hadi kufikia sasa kukiri na kutakasika kunaofatia vimehusika pia kwenye njia inayojulika. Hata hivyo, 1Jn.1: 9 yahusu dhambi ambazo tayari zimetendwa, na sio na kiini (nafsi) ambacho kinaanzia, “Dhambi zetu zinashughulikiwa na damu, sisi wenyewe tunashughulikiwa na msalaba. Damu hutengeneza msamaha wetu, msalaba hutengeneza ukombozi kutoka kwa kile tuko ndani ya Adamu. Damu yaweza kuosha dhambi zangu, lakini haiwezi kuosha mtu wangu wa zamani: Ninahitaji msalaba unisulubishe – mwenye dhambi.”

MAARIFA:

Leo mojawapo ya majaribu ambayo yameanza kwa ajili ya kitu kizuri ni kwenda ndani hadi kwa “Ubatizo wa Roho.”Kuongea kwa ndimi, n.k Huu ndio kwa kweli mtego ambao ni hatari na kusikitisha sana kuliko mingine, jinsi ilivyo nafsi tuu, isiotulia na kuenea kidini. “Kalvari hutangulia Pentekoste. Kifo na Kristo hutangulia

Ukamilifu wa Roho. Nguvu! Ndio, watoto wa Mungu wanahitaji nguvu lakini Mungu hapeani nguvu kwa viumbe vya zamani, wala sio kwa nafsi ambayo haijasulubishwa. Shetani atampa nguvu yule ‘Adamu wa zamani; lakini si kwa Mungu.’

Nani kati yetu asiyejua kitu kuhusu kutofaulu kwa njia zetu, wanaodhamiria vizuri vile wanavyoweza? Lile wengi wetu wasilolifahamu ni nini huku kutofaulu kwenyewe kulivyo njia ya kujifunza, na kuingia ndani, njia ya Mungu. “Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA.Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.”(Isa.55: 8,9). Sasa ni njia gani ya Mungu ya kujikana? Ana njia moja tu, na iko kwenye msingi wa njia zake zingine zote: kanuni ya kazi iliyokamilishwa. Njia yake kwetu katika kila kitu ni njia ambayo tayari amesafiri, shinda, na kukamilisha katika Kristo.

NJIA YA MUNGU:

Ulikuwa msalabani pale Kalvari ambapo Mungu, katika Kristo, alishughulika vikamilifu na nafsi, asili ambayo kutoka kwayo dhambi zetu zote hutiririka. “Mkijua neno hili ya kuwa utu wetu (haujabadilishwa) wa kale ulisulubishwa pamoja naye ili mwili wetu wa dhambi, (ambao ni chombo) tusitumikie dhambi tena.”(Rum.6: 6, kwa upana) sababu hakuna njia nyingine kwa utu kukanwa ni kwamba Mungu amefanya kazi kupitia njia

hii: kujitambulisha kwetu kwa Kristo Yesu katika kifo chake na ufufuo! Imefanyika; sasa letu ni kuamini.

“Mwili utujipeana tu msalabani; sio kwa kauli zote ambazo mwazitengeneza kwenye mkutano, si kwa nguvu zozote za kibinafsi, si kwa jaribu lolote la kujisulubisha mwenyewe; kwa kusaidiana kusulubishwa, kusulubishwa pamoja na Kristo. (Gal 2:20)

Si kwa kujiweka wewe mwenye kifoni, bali nikiwa kuchukua, kwa imani na kujipeana, nafasi yako ya ushirikiano na Kristo katika kifo chake. Hiki ndicho kizuizi cha usalama kilichobarikiwa kati yako na mivutio yote ya mwili, na hiyo hufungua njia ya kutenda mapenzi ya Mungu “(G.Watt).

Msalaba wa Kalvari ulisababisha kifo cha Bwana Yesu, kwa ajili ya dhambi, na kutenda dhambi. Katika hiyo alikufa kutenda dhambi, alikufa kutokana na milki ya dhambi, na alifufuka katika milki ya “upya wa uhai,” uzima wa milele. Na kuthibitishwa kwetu naye pale Kalvari kulitufikisha kifoni: chini hadi kwenye kaburi; juu hadi kwenye “Upya wa maisha.” (Rum 6:4). Kwanza, Warumi 6:4 –“Kuzikwa naye”; halafu, Warumi 6:5 – “Kwa maana kama mlivyounganika naye
katika mfano wa kufufuka kwake,”Pia, Wakolosai 3:3 –“Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja Kristo katika Mungu”; Kwa hivyo, Warumi6: 11 – “Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu bwana wetu.”

Msifuni Bwana! Yote yalitendeka pale Kalvari dhambi zetu zililipiwa, hali yetu ya dhambi ilishughulikiwa, na yote ya - kifo. Na tunapata faida ya kazi ya msalaba kupitia tu kuhesabu, kuamini katika,
kazi iliyomalizika ya msalaba. Kwanza, kupitia kwa neno, tunapata yale Mungu alifanya kuhusu shida yetu. Halafu, jinsi tunavyoelekea vilivyo kushawishika kwa ukweli na kuanza kuelewa vyema, tunaweza kukubali “kujihesabu” ni kweli. Na jinsi tunavyojizoesha imani katika ukweli wa Mungu, tunaanza kupokea faida ya ile kazi iliyomalizika katika ujuzi. Haikuwa kweli katika swala la kuhesabiwa haki? Ndio, na vivyo hivyo nasi tutapata kuwa kweli katika swala la uhuru wetu kutoka kwa utumwa wa maisha ya utu.

“Matokeo yenye nguvu ya msalaba ni Mungu, mbinguni, katika ondoleo la makosa, na ushirikiano mpya na Mungu, ni ule ambao hausambaratiki kutoka kwa matokeo mengine – kuvunjika kwa mamlaka ya dhambi kwa mwanadamu, kupitia kwa kusulubishwa kwa utu. Kwa hivyo neno litafundisha kwamba msalaba haufanyi kazi tu tabia au shauku ya kutengeneza kafara kama hiyo, bali hutoa kwa kweli nguvu ya kufanya hivyo, na humaliza kazi. Hili laonekana pamoja uwazi wa ajabu katika Wagalatia. Katika sehemu moja msalaba umesemeka kama upatanisho kwa makosa (3:13). Lakini kuna sehemu tatu zaidi ambazo msalaba umeongelewa kwa uwazi zaidi kama ushindi juu ya nguvu za dhambi kama nguvu za kusimama katika sehemu ya kifo “Mimi” cha maisha ya utu;ya mwili (Utu unaotekelezwa zaidi);na ya ulimwengu (2:20;5:24;6:14). Katika taarifa hizi ushirikiano wetu (uthibitisho) na Kristo, aliyesulubishwa, na kugeuzwa kama yeye kunatokana na umoja, vimeletwa kama matokeo ya nguvu zilizoonekana ndani yetu na juu yetu na msalaba.”(Anderea Murray).

Kama vile tunavyojifunza kusimama kwa kazi iliyomalizika ya Kalvari, Roho Mtakatifu ataanza kwa imani na kwa ukamilifu kutumia kazi hiyo iliyomaliziwa ya msalaba kwa maisha ya utu, kupitia kwa hayo kukaa imara katika sehemu ya mauti – yenye kimya – husababisha “Si mimi, bali Kristo”maisha.

## SURA YA 12
## MSALABA

Kusoma kuhusu ukweli huu ni kazi ngumu, si ni hivyo? Ijapokuwa njaa ya kiroho na hitaji ni masharti makuu ya mwanga na kutambua, Roho Mtakatifu haachilii hazina za dunia kwa haraka au kwa urahisi. “Kina huita kwa kina.” Ni lazima tujitayarishe, na hata hivyo kuna muda wa kutosha, kuchimba, kuomba, kuwazia, kutamani na ujuzi unaowekelewa. Kuwepo kwa ukweli wa maisha ya kiroho huja sio kwa njia nyingine, ila Msifu Bwana, inakuja kwa njia hii!

Kuelewa na kusawazisha kiini cha maneno ya mambo ya msalaba hutokea kuwa mambo yaliyo magumu na ya majaribio kwa yote katika maisha ya mwumini ambaye anaendelea kukua. Bwana wetu huweka kwenye ghala lake yaliyo mema na ya thamani kwa ajili ya wale ambao wanamaanisha kumtumainia, wale wanao kiu na njaa kama ilivyo katika Yesu Kristo.Ufahamu wa mwumini kuhusu haya mambo mawili ya Kalvari yaani; ukuaji wa kiroho, na huduma inayopeana maisha.

Kalvari ndio siri yake kamili. Ni kile alitenda pale kinachohesabika, na kile alichofanya pale huwa ni nguvu katika maisha ya mkristo ikisawazishwa na imani. Hapa ndipo maisha yote ya ki-Ungu huanzia ikiinuka. Hatuwezi jua ushindi wa Kristo katika maisha yetu hadi tutakapoelewa ushindi wake msalabani ndio siri ya ushindi wetu binafsi katika maisha ya leo. Hatuna ushindi wowote kwetu wenye haukukuwa wake mwanzoni. Chochote tunatarajia ni kile alichonunua, na kile alichotununulia tunapaswa kumiliki. Mwanzo wa maisha matakatifu ni imani katika Mwokozi aliyesulubishwa ambaye anaona zaidi ya kazi yake aliyofanya kwa niaba yetu. Ni imani inayoona mimi nikiwa pamoja na Kristo katika kifo chake na kufufuka kwake.”

Hakika, Baba Yetu ameagiza kila mmoja wetu kwa njia pekee isio ya mkato wa imani katika kanuni hii ya pili ya Kalvari: Kujitambulisha kwetu kibinafsi na Kristo katika kifo chake kwa ajili ya dhambi hadi ufufuo. Hili agizo lilitufundisha kuhusu kiwango cha kwanza: Kusadiki na kusawashisha kazi iliyokamilifu ya kufa kwake kwa ajili ya dhambi zetu – kutuweka haki. Basi tumeulizwa bila shaka kusadiki na kusawashisha sehemu ijayo: “Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, “Warumi 6:6a); “Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.” (Warumi 6:11a)

Hekima tuliyosimama nayo kwa imani kuhusu ukweli wa Kalvari huweka Roho Mtakatifu huru kuleta kazi ile iliyokamilifu kwa maisha yetu ya kila siku. Tulisimama kwenye msingi wa kifo chake kwa ajili ya dhambi zetu, na tendo hili la imani iliruhusu Roho Mtakatifu kutuletea uhuru kuepukana na kujilipia deni la dhambi – kuwekwa haki. Mara tu, tunapofikia ukweli huu mwingine, tumeulizwa kwenye Neno kusimama juu ya ukweli unaoleta huru wa kufa kwetu pamoja na Kristo katika kifo chake kwa dhambi, inayoruhusu Roho Mtakatifu kuleta katika maisha yetu huru kutokana na nguvu, na ufungwa wa dhambi katika maisha yetu -utakaso unaonawiri. Na bila shaka twasimama Naye katika utukufu, milele tutakuwa huru kutoka katika uwepo wa dhambi – tukiwa tumetakaswa na kutukuzwa kamili.

“Kama aliyechukua sehemu yetu kufa/kwa niaba yetu alienda msalabani pekee, bila sisi; na hapo, machoni mwa Mungu, sisi sote tulikufa pamoja na Kristo. Twaweza kusamehewa kwa sababu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu; Twaweza kombolewa kwa sababu tulikufa pamoja Naye.

Njia ya Mungu ya kutukomboa sisi, kisasi chenye kutoamini isiyotibika, sasa inaondolewa msalabani mwa mwanawe, na kuweka mwanzo mpya kwa kutuumba mara nyingine kwa njia ya kutuunganisha pamoja Naye, Aliyefufuka, Aishiye (2wakorintho 5:17). Ni Roho Mtakatifu ndiye atakayefanya haya maneno kuwa sawa na kweli kwetu tutakapomkubali; Basi shida za mioyo yetu yatatulizwa, na tutabadilishwa kuwa jinsi Kristo Alivyo.

“Kupitia kusulubishwa kwa utu wetu wa kale pamoja na Kristo Mkristo/mwumini amefanyika kufa kwa dhambi, amekuwa huru kabisa kutokana na nguvu za dhambi, amechukuliwa mbali na hali ya dhambi ya kukwamilia watu, sehemu ya dhambi maishani mwake imevutwa. Huu ndio kutwaliwa kwa neema ya Mungu usio na mawa lakini hii inaweza kuwa wa maana kwa maisha ya mwumini atakaposhikilia imani kila mara, kila siku, ijapokuwa majaribu yanamkumba, ‘kulihesabu’ kuwa kweli. Anapolihesabu Roho Mtakatifu Anaendelea kuliweka kuwa kweli kwa wazi anavyoendelea kudhania, Roho mtakatifu ndivyo anavyoendelea kufanya kuonekana kweli. Dhambi haingetaka kuwa na nguvu nyingi dhidi ya aliyeamini kuliko vile yeye huipeana kupitia kwa kutokuamini. Iwapo yu hai kwa dhambi itastahili kwa kiwango kikubwa kufatana na kanuni kwamba ameshindwa kujihesabu mwenyewe katika dhambi. “R. Paxson.

Mabadiliko yameleta mkazo machoni kwa mara nyingine pasipo hiyo hakuwezi kuwa na mwanzo. Kinachokosekana miongoni mwa waanio siku hizi ni mkazo halisi juu ya ukuaji- sio kuokoka tu, na halafu mbinguni. Ni aina ya wokovu ambao tunaweza kuwa nao ikiwa Baba yetu alituokoa tu kutokana na deni la dhambi zetu, na hatimaye tukabiliane sisi wenyewe na nguvu za dhambi katika maisha yetu ya Ukristo na kutembea? Lakini baadhi ya kadiri aliyoenda, na sisi tunajikakamua kupata mema wanayoweza pamoja na msaada wake. Na hili ni kosa la wagalatia, linaloonekana wazi hata sasa. Kote katika maisha ya kuzaliwa upya. Ni lazima turudishwe kwa kanuni mbili; Kuwekwa huru kutokana na nguvu za dhambi kupitia haki kupitia imani---“(Gal 3:24)”--- watembee kwa imani –“(Gal 3:24)” – tuatembea kwa imani “ (2 kor 5:7); “Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, endeni vivyo hivyo katika yeye” (kol 2:6)

“Hatujaachwa sisi wenyewe kushughulika na maisha ya zamani; imetekelezwa na Kristo msalabani. Huu ni ukweli ambao wapaswa kujulikana. Huu ni ukweli ambao wapaswa kujulikana, na juu ya huo ukweli kumejengwa kanuni za Agano Jipya na mafundisho ya utakatifu. Kwa njia nyingine, kalvari ni msingi wa utakapo vile vile wa kuhesabiwa haki. Vipawa hivi vyote viwili huchipuku kutoka kwa kazi ile ile na ni hizo hali mbili za wokovu uo huo”

Kwa hivyo, kadiri ya muamini hatambui hali hizi mbili kuuu za wokovu wake, lililo njema la kufanya ni kutafuta tubu (1 Yoh 1:9) maana yake, baada ya uharibifu kutendeka! Hili linashughulikia adhabu ya tukio hilo, lakini sio chanzo, si wakati tulimuidhinisha Roho mtakatifu kuingia katika chanzo, na kukata mto huu wa dhambi

kabla hazijatendwa? Si hili bora zaidi kuliko uharibifu ulioletwa na dhambi, hata kama zimetubiwa? Wakawaamini wanakuwa wagonjwa na kuchokeshwa na mzunguko wa mwaka baada ya mwaka katika kizimba cha kulishwa kiroho- kutenda dhambi, kulingana, baadaye kutenda tena- watakuwa tayari kwa jibu la Mungu kuhusu chanzo cha dhambi, ambacho ni kifo kwa nafsi kilicholetwa na kazi iliyokamilika ya msalaba.

"Wakati mwanga wa Mungu huangaza kwanza katika nyoyo zetu kilio chetu kimoja ni cha msamaha, kwa kuwa sisi hutambua kwamba tu wenye dhambi mbele yake; lakini pindi tu tunapojua msamaha wa dhambi, tunafanya uvumbuzi mpya- uvumbuzi wa dhambi, na tunatambua kwamba tuna asili ya mwenye dhambi kuna kule kuelekea kwa dhambi kwa kindani. Kuna nguvu za kindani zinazotuvuta kuingia kwenye
dhambi, na wakati nguvu hizo hulipuka tunatenda dhambi. Tunaweza kutafuta na kupata msamaha lakini hata hivyo tunatenda dhambi tena; na maisha huendelea hivyo kwa mviringo mbaya- kutenda dhambi kusamehewa, ingawa hivyo ni kutenda dhambi tena. Tunashukuru kwa msamaha wa Mungu, lakini tunahitaji kitu zaidi ya hicho, tunataka ukombozi kutokana na jinsi tulivyo"

"Kudhani kwetu juu ya kazi iliyokamilishwa ya vifo vyetu katika dhambi, ndani ya Kristo pale Kalvari, ni njia moja ya Mungu ya ukombozi- hakuna njia nyingine kwa sababu hivyo ndivyo alitenda. Tulijifunza kutokuongeza kwa kazi iliyokamilishwa katika swala la kuhesabiwa haki, na sasa ni lazima tuifunze kutoongoza kwa kazi iliyokamilishwa ya kuwekwa huru. Tutawekwa huru wakati tutakapoingia katika uhuru wake uliotayarishwa- hakuna kwingine. "Mwamini hawezi kamwe kuushinda utu wa zamani hata kwa nguvu za yule wa sasa mbali na yule wa sasa na kwa hivyo kifo cha Kristo katika dhambi ni lazima, na hadi msalaba utafanywa kiini ambacho kwacho huushinda utu wa kale, hutumbukia tu katika muundo mwingine wa maadili mema; kwa maana nyingine, anatafuta kwa nguvu zake binafsi kushinda nafsi yake, na mapambano ni yasiyo na matumaini"- C. Usher.

Marcus Rainford alikataa kutamatisha upungufu wa uhuru asili wa Mungu "Haitakikani kuwa maono ya akili yanayopita tu wakati hatusumbuliwi mpangilio wa furaha tu wakati tuko chini ya matulizo yaliyo ya kudumu kutoka kwa uwepo wa Bwana si akili ya kujisifu mno kwa moyo ambayo umejaribiwa katika kazi njema; si kutoka kwa hayo yote muamini anaweza kuona uwezo wake wa kimatendo juu ya dhambi, lakini kwa misingi kwamba Kristo alikufa katika dhambi na anaishi kwa Mungu kupitia Yesu Kristo Bwana wetu".

"Ni lazima nitambue kwamba adui ndani ya kambi- mwili, utu wa kale, nafsi, mimi, Adamu wa zamani- ni usultani. Kwa imani ni lazima nimuhesabu yeye kuwa katika sehemu ile Mungu alimweka- kusulubishwa na Kristo. Ni lazima nitambue kwamba sasa maisha yangu yamefichwa na Kristo katika Mungu; kwamba yeye ni uhai wangu"- Ian Thomas

# SURA YA 13
# KUMI NA TATU
# UFUASI

-Mfuasi ni yule ambaye hueleza kwanza ushirika wa msalaba, ambao huleta ushirika na Bwana wake: ufuasi. “Upatanisho wa msalaba na ushirika wa msalaba ni lazima uhubiriwe sawa kama sharti la ufuasi halisi” Kristo ni jibu, lakini msalaba watakikana kusafisha njia yake”

Katika maendelezi ya kiroho, Bwana wetu hasukumi, Yeye ni kiongozi wa safu ya askari (Wah 12:2), na anatuongoza hatua kwa hatua. Tunapambana na hatufaulu (nguvu za kibinafsi), ambazo huleta hamu kwa jibu kwa huku kushindwa kwa kusikitisha. Katika wakati, tunaona ukweli wa kibibilia wa ukombozi katika msalaba (utambuzi), na huo baadaye huleta njaa inayohitajika kuingia katika ule uhuru, uhuru wa kushiriki na jibu- Bwana wetu aliyefufuka.

“Hakuna kinachoweza kututenga kwa Mungu, hakuna kinachoweza kutuweka watakatifu, isipokuwa jinsi msalaba unavyofanya kazi ndani yetu kwa sababu msalaba pekee waweza kuweka vizuizi kwa utakatifu katika nafasi ya kifo”- G Watt, Nyuma ya kazi yote ya mafanikio kwa waliopotea ni mapigo ya ndani ya kiroho; na nyuma ya mapigo ni Roho Mtakatifu ambaye huzaa Kristo ndani yetu; na alama mpya ya yote ni msalaba, hali ya kuishi tunayopitia ambayo lazima yote yaingie na yaongoze maisha kabla hatujawa sawa kwa ajili ya huduma”- J. E. Conant.

Hakuna mahali popote pale bwana wetu Yesu alikuwa wazi na imara kuliko wakati alipotaja ufuasi. “Akawaambia wote, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajifuate----- Na mtu yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu” (LK:9: 23, 14:27). Sababu yake kwa haya ni wazi; Nafsi hawezi na hataweza kamwe kumfuata, lakini kuchukua msalaba wako mwenyewe huleta kifo kwa nafsi, na upya wa maisha katika Yesu Kristo.

Mfuasi ni yule ambaye yuko huru kutoka kwa ukale, na huru kwa upya. Katika maneno mengine ya kibibilia; Wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu” (Rum 6:11). Na kwa hili Bwana Yesu asema kwamba kila mmoja sharti achukue msalaba wake. Hapa ndio mwisho, kwa hivyo sasa kwa jinsi gani. Lakini kwanza, kwa nini sio kuchukua msalaba wako. “Wakristo wapaswa kuelewa kwamba kuvumulia msalaba, lakini kupeana maisha kwa kila siku, kwa kufa kwa nafsi ambako lazima tutupe alama jinsi

Hakuna kazi halisi ambayo itaanzishwa bila kuwa na akili ya hitaji ambayo itaundwa. Hatuwezi kuipenyeza hiyo ndani ya wengine; Sisi hatuwezi ulivyofanya Bwana Yesu, ambayo tunahitaji wakati wa kuimarika karibu zaidi ya taabu, na bila hiyo ukamilifu wa baraka ya msalaba haiwezi kudhihirika kwetu”- Andrew Murray.

“Sharti tukome kuchanganya maneno na kwa wakati mwingine waamini katika kujisikitikia wenyewe hujihuzunisha enyewe, na kusema, ‘Nimechukukua, au lazima nichukue msalaba wangu, na kufuata Yesu. Kama lingekuwa hilo ambalo tungepoteza kuona ‘msalaba’ wetu, katika msalaba wake, basi msalaba wake ungekuwa msalaba wetu; kifo chake, kifo chetu; kaburi lake, kaburi letu; kubadika kwa maisha yake,

maisha yetu mapya", La, kuchukua msalaba wetu hakumaanishi kutojali kubeba mzigo mzito, ugumu, magonjwa, hali au ushirikiano ambao hauonjeki. Kuvumilia kitu havijumuishi msalaba wetu.

Msalaba wa muamini ni msalaba wa Kalvari, msalaba ambao alisulubishwa nao Kristo ( Gal 2;20). Pale kutangaza kuwekwa huru kwa milele. Kulitiwa sahihi na Roho wa Mungu. Kila muamini basi aliwekwa huru kutoka kwa utumwa wote, lakini kila muamini hana habari kuhusu ukweli huu unaoweka huru.

Yahuzunisha kusema, waamini wale pekee yao wana shauku katika kuwekwa huru ni wale ambao wamekuja pahali pa kuchukiwa badala ya kuanika minyororo yao. " Ni ukweli kwamba akili imezuoliwa na msalaba; bali ushindani kwa msalaba ni haswa uadilifu, kwa mwenye dhambi na katika mtakatifu, kwa kuwa ujumbe wake umekaribishwa tu na wale ambao wanatamani uhuru kutoka katika utumwa wa dhambi, na wenye njaa na kiu baada ya haki ya Mungu anayopitia. " Ndio, hitaji lazima liwe kubwa jinsi Norman Douty anavyosema; "Njia ya Ki-ungu (kupitia msalaba) ya kuwekwe huru kiroho ni kama usumbufu kwa mtoto wa Mungu kama vile njia ya Kiungu ya wokovu ni kuja waliopotea".

Wakati muamini atakapo kweli kuona msalaba namna ulivyosehemu ya kifo- anachukua mwelekeo wa kuchelewa wa kuchagua uhusiano kama huo. Bwana wetu Yesu anaelewa haya vyema, lakini hakuna njia nyingine, kwani hiyo ndio namna alivyokamilisha kazi kwa niaba yetu. Kwa hivyo Yeye usipopoa hadi wakati tunainamia lazima yake.

Tutakuwa tayari kuchukua msalaba wetu wakati usisi unakuwa hauwezi kuvumiliwa kwetu, wakati tunapoanza kuchukia maisha yetu-" na usichukie --- maisha yake mwenyewe--- hawezi kuwa mfuasi wangu "(Luka 14: 26). Mzigo mzito wa nafsi na njaa ya kuwa kama Yeye unafanya matumizi ya msalaba- kusulubishwa- kuwa wa kuvutia. Miaka mingi ya uharibifu ya utumwa hafifu hufanya uhuru katika bwana Yesu usio na bei-gharama huwa kama si kitu kwetu! Fikiria kuhusu hilo, sisi huanza kushiriki fikira za Bwana wetu Yesu, na za Paulo. 'Kwa kuwa furaha ambayo iliwekwa mbele Yake", Bwana Yesu " kwa subira ili vumilia msalaba" (Heb 12:2, Wey.). Fikira za mtume Paulo ilikuwa; " Lakini Mungu anakataza kwamba nipeane utukufu, katika msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo' "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu" ( Fil 2:5). Ndio, tunaanza kutukuza ndani ya msalaba, uhuru wetu wenyewe kutoka kwa utumwa wote ule, kutoka kwa yote ambayo yanaweza kutuweka mbali na ushirika na bwana wetu aliyefufuka. Kwa hivyo tunaanza kuchukua msalaba wetu, uhuru wetu, kazi yetu ya kibinafsi iliyokamilishwa ambayo imeshikwa katika tumaini kwetu kwa muda mrefu na kwa uvumilivu na Roho mtakatifu. Ongea kuhusu hazina za tumaini zako!

Hivi ndivyo tunachukua na kubeba msalaba wetu; Hatimaye kutayarishwa na mahitaji yetu, kuwa na habari kuwa utumwa wetu ulivunjwa ndani ya Kristo pale Kalvari, tunaanza tu kutumainia kwa kazi ile iliyokamilishwa- tunatwa. Nia yetu huwa; ninachukua kwa furaha na kwa hiari, kwa imani katika kweli, kazi yangu iliyokamilika ya kuwekwa huru ambayo ilianzishwa pale Kalvari; ninajihesabu mimi mwenyewe kuwa mfu kweli katika dhambi, na hai kwa Mungu katika Kristo. Huku ni kuchukua

msalaba wako. Vile tunavyojifunza kufanya hili, tunaanza kupata kweli kweli hizi kuwa za kuamika katika hali tunazopita. Roho mtakatifu huleta kazi ile iliyokamilishwa ya kifo cha Kalvari. Iwe na wakati tunaenda mbali na kweli na kuanza kuegemea kwa kitu au mtu mwingine pamoja na sisi wenyewe, nafsi inaachiliwa kutoka kwenye msalaba Kwa nguvu na kuwa utumwani kama hapo awali. Kupitia kwa njia hi,i tunafunzwa kwa subira kutembea kwa imani, kudumisha nia yetu ya kutegemea kwa kazi iliyomalizwa ya msalaba.

Adolph Saphir aliandika, “Njia nyembamba, inayoanza na mslaba- ‘Mmekufa na Kristo- inayomalizika na utukufu wa bwana Yesu, ni njia ambayo Bwana huileta karibu na kutembea na wafuasi wake.“Kristo yu aishi ndani yangu”. Bwana wa ndani huishi kama chanzo cha kipeke cha maisha. ‘Mimi’ wa kale hana mchango ambao anaweza kutoa katika maisha ya ukristo na huduma; hawezi kufungwa nira na kusudi la Mungu. Kifo ni sehemu yake iliyoamrishwa. Hakuwezi kuwa na mabwana wawili katika maisha yetu. Kama ‘ mimi’ wa kale ametumiliki kwa nguvu basi Kristo hawezi kuwa. Lakini kama tutachukua ukweli mkuu wa ukombozi kwa furaha- ‘Nimesulubishwa na Kristo’- basi Kristo kwa Roho Wake huchukua zoezi la matumizi ya maisha ndani yetu, na hutuongoza kama watumishi wake (wafuasi), katika gari lake la ushindi.

## SURA YA 14
## KUMI NA NNE
## NJIA YA UFUASI

Katika hadithi ya mpanzi, mbegu iliyopandwa “Kwenye mchanga mwema ni wale, wanaposikia neno, hulihifadhi, na huzaa matunda kwa uvumilivu” Luk: 8:15). Kanuni ya ukuaji daima,

“Kwanza kujipuka, halafu suke, baada ya hiyo ni nafaka nzima ndani ya suke” {Mk 4:28]. Kwa hivyo, “ mkulima husubiri tunda la thamani la mchanga, na amelingoja kwa uvumilivu”( JM 5:7). Kama vile inavyoonyesha wazi kwa mfano, “ Yule anayeamini hataharakisha” ( Isaya 28: 160.

Kwa kuwa wengi wetu umekuwa muda mrefu wa ukuaji kuanzia chembe ya jani hadi “ mbegu nzima ndani ya suke”. Kwa hivyo wengi hutafuta kukaa kwa hatua hii; waliokoka, pamoja na hakika ya mbinguni- Kuongezea kipimo cha kuridhisha cha jukumu la ukristo, ikiwezakana kwenye mienendo ya kikanisa. Hapa kuna muamini kama vile kiini cha ngano ambacho kimebeba uhai ndani ya kisetiri cha kidhahabu kinachometameta, katika ushirikiano kwa shina na kiini hicho hicho cha ngano. Hii ni hatua tu, sio lengo. Na, kama umri wa kati hii linaweza kuwa hatua ya hatari; ile ya kutafuta kutulia ‘ kunakofaa zaidi”; ya kuota bila sababu katika ushirika wa mikutano, madarasa, n,k.; ya kiujinga au kusahau mapambano na kukua kwa uchungu kwa kijani kidogo kwa mtu yeyote, na kutarajia na kuwausia kwa kuwaweka sawa na kukomaa bila kuchelewa.

Hii yote ni saha, lakini ghali ni kukaa vizuri, lakini haina mazao. “Mbegu ya punje yaweza kuonekana nadhifu, lakini ni ngumu. Kiini cha uhai kimefungiwa ndani ya kombe lake na haiwezi kutoka nje. Kwa hivyo haitoi kitu chochote. Hapa kuna sababu inayonyesha kwa nini wakristo wengi, hata wahubiri, hawazai matunda. Utakuta tu mmoja hapa na pale ni mwenye kufanya watu warudi kwa Kristo. Wakati nafaka inapozikwa mchangani inakufa na ile sehemu ngumu huwa rahisi na kuoza ili ipeane miche changa na ndogo na apate chakula na kumea kama hii haijafanyika mimea itakufa tena haiwezi kukua

Kila mtu mpaka ajiesabu kufa kwa ubinafsi ngumu tena baridi kama barafu ambaye ni “Mimi” anaye. Kwa hivyo nguvu ya Roho mtakatifu ambayo inanyorosha vitu atatenda kazi akitakasa Wakristo katika kazi ya Mungu. Watu wengi watataka wadumu kwa kazi ya Mungu na hawawezi kwa sababu ya hali ya mwili yao maishani mwao.

Baba yetu anajua haya yote, na tena yeye ndiye anafanya haya yote anaweka, mbegu kuwa na moyo kuwa haistahili,na tena anatuonyesha kwamba kuna mahitaji mengi maishani mwetu kuzidi kiwango cha kuwa na uokovu peke tena kuwa na ukomavu kwa ajili yake. Tena ni kitu ambacho kinahitajika kwetu ili tubadilike tutoke katika kuwa mkristo ambaye maisha yake iko duniani na tuwe wakristo ambao wana mazao katika njia za Mungu ambazo anazitumia akimchagulia kila mmoja tukiwa katika mkono wa mkulima hatuna uoga na tuko huru.

“Tunaweza kupata mkristo ambaye ana ujuzi mwingi tena ana hekima ana nguvu tena ana tabia nzuri, na tena anaweza kuwa na hekima ya hali ya juu –Ukitazama mtu

kama maisha yake na nguvu yake ya kibinadamu ndiyo inaonekana. Uzuri wa Mkristo huyu unakuwa mgumu tena anapinga wengine katika uzuri wao. Kuna dalili ya kila aina katika maisha yao ya kila aina katika maisha yao ya kuwa watu wema –na kitu ambacho hawana ni kwamba hawajasulubiwa ambacho kitawaandaa ya kipekee na neema ambayo haina kipimo kwa wengine.

“Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake “Akajibu, akisema, azipandaye zile mbegu njema ni mwana wa Adamu lile konde ni ulimwengu zile mbegu njema ni wana wa Mfalme ya yale magugu ni wana wa yule muovu Mathayo 13:24,37,38

Bwana mvunaji anapanda, anafunika Wakristo kama mbegu shambani ambayo ni dunia.

Kwa unyenyekevu wa mkulima na mapenzi yake anayependa naye kazi hii ya ukulima, mbegu ndogo ambayo iko juu ya mti ambayo imebeba mimea atakuwa na uoga kuzivuna tena kuziweka pamoja kwa hivyo ataanza kuwa na njaa itakayo zaa matunda mengi hii ndiyo njia ambayo Mungu anatumia kuhimiza wafwasi wake, hii ni mahitaji muhimu ya moyo ambayo ni njaa ya kuzalisha matunda

Ataomba awe na mazao na njia zote na atapata Bwana akisema “Ami, Amin nawaambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi ikafa hukaa hali iyo hiyo peke yake bali ikafa hutoa mazao mengi (marko 8:35) tukiwa na majibu kuhusu njaa hii basi Roho mtakatifu ataanza kufungua mbegu ya mimea mahali pazuri anapo kisiri siri na pole kama mimea imekuwa tayari mtu huyo atachukuwa kisu chake cha kuvuna bila kukawia na kuanza kuvuna kwa sababu wakati wa kuvuna umefika” (marko 4:20)

Mwishowe hivi karibuni hata mbali mbegu ya mimea itajipata ikianguka mpaka chini kwa mchanga mahali penye baridi tena penye giza tororo. Tena kitu kibaya zaidi itakuwa usiku na kulimaliza koti lake la dhahabu nzuri tena kilicho kibaya zaidi koti hili litaanza kuoza na kuanza kuanguka na kutawanyika vipande vipande. Kitu ambacho hakiko kwa Kristo hata ingawa ni kizuri kiasi gani ikiangaliwa kusemwa- hali yake itaonekana vyema vile alivyo kwamba ni kazi ya kimwili. Bado kutakuwa na kitu ambacho kitaendelea kuturarua mno ikitupeleka chini zaidi katika kifo. Hili ni jambo kuhusu mbegu ya mimea ambayo ina utulivu.

“Tazama utaniua sina tumaini ila hata hivyo nitaithibitisha njia yangu mbele yake Ayubu 13:15)

“Kama haitaanguka chini na kufa
Je, mazao mengi yanaweza kuja kwa thamani kama hiyo?
Mbegu ya Mimea mpaka ifunikwe chini
Furaha ya mvua ya masika imekwisha?
bado mbegu inazikwa hapa na pale
Wale wanaokuja wanaweza kunywa kikombe chake
Kama haitaanguka chini na kufa?
Je mavunoyo siku, zijazo yatakuwa aje?
Mazuri, na wewe pia unasaidia kwa mavuno hayo

Kwa yule ambaye ametupa maisha yake wacha ife

Na ukilitupa hivo utapata maisha mapya
Kristo anatufunulia uso wake ambayo umejaa
Upendo na utukufu wake unayo ng'ara kama kioo
Utakua kwako

Mkristo akichukua msalaba wake kufuata Kristo hatua ya kifo mpaka ianze mfuasi wa Yesu huyu atajipata akiwa mbegu ambayo imepandwa nyumbani ofisini, hospitalini, kanisani hata katika msheni. Hata ikiwa ni nini au wapi ambapo mkristo amepandwa mfano wa kifo itapita kwake ndiyo baadaye atakuwa na maisha ya ufufuo "Kwa maana sisi tulio hai siku zote twatolewa tufe kwa nao udhihirishwe katika mwili yetu ipatikanayo na mauti 2Wakorintho 4:11-12.

Inahitajika tuwe kwa kina katika ukweli kwamba mwana wa Baba anayempanda hangeingia katika utukufu wa mbinguni kabla ya kujikabidhi kwa kifo na ukweli mkubwa hii inapotufungulia njia itatusaidia ili tujue kwamba katika maisha yetu tena kwa kuwa na ushurika na Kristo ni kitu kigumu ambacho haiwezekani tuionje maisha hii na Kristo kabla hatujajikabidhi na mienendo yetu na tabia zetu zote kila siku ili sheria na dunia ndiyo baadaye milele kama wafuasi wa Kristo tukiwa na Bwana aliyesulubiwa msalabani baadaye akafufuka PS"Ukweli yote tumeshasoma juu ya msalaba kwa kukufa kwetu, kukufa kwake vile mbegu ya mimea inaanguka chini ili ife ndiyo njia ya maandalizi ya kushinda maisha haya ndiyo msingi, tena ndiyo mambo yanayotakikana zaidi katika maisha

## SURA YA 15
## KUMI NA TANO
## KUPUMZIKA

“Kupumzika mapumziko yanayobaki kwa watu wa Mungu wanayoweza kupata kwa sababu mtu akienda kupumzika na Mungu atawacha kazi yake mwenyewe ili apumzike vile Mungu pia alivyowacha kazi zake akapumzika kwa hivyo tuwe na bidii ili tuingie katika mapumziko hayo (Waebrania 4:9-11a) Maneno mengi yanayo leta uzima katika Bibilia yamebeba maneno mawili yanayo shikamana ambayo hayawezi kugawanywa. Kwa hivyo tuwe wenye bidii tuingie katika mapumziko kwamba mpaka tujaribu tukitafuta, na kuomba tena tunakuwa na moyo wa uchungu katika kiwango cha kugundua na kufahamu ukweli unaohusiana na mahitaji haya. Tena katika safari hii tutatembea kwa uchovu tukijaribu kuchukua na kuingia katika njia zake. Haya hayafanyiki bure, ni kitu ambacho kinahiatajika na sio mapumziko ni kufungua kunakotuingiza katika mapumziko halisi.

Ni kitu muhimu kinachoonyesha mioyo ya watu kupitia katika kiwango cha kupiga vitu ili tufike katika ukweli unao takikana baadaye tunakuwa na hakika juu ya maneno haya, tunaanza kugundua vitu vyetu ndani ya Bwana wetu Yesu Kristo tunavyoambiwa katika Biblia “Kwa maana Bwana MUNGU, mtakatifu wa Israeli asema hivi, kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini lakini hamkubali (Isaya 30:15) Ni heri tuwe na utulivu tukiwa na nguvu tukitazama Baba wetu tukiwa na ujasiri. Kwa tumaini tunayo kwake, tena tunamshukuru kwa yale ambayo ametupa kwa mwanawe

“Hao wote wanakungoja wewe’ uwape chakula chao kwa wakati wake, wewe huwapa, wao wanakiokota wewe waukunjua mkono wako wao wanafadhaika (Zaburi 104:27-28)

Norman Grubb anatufundisha kwa jambo jema Isa mpangililio ya kuwa na mapambano na mapumziko. Chakula kwa mfano kujifundisha lugha gani, utakutana na aina ya picha katika kitabu yenye maana fulani, utasikia sauti inayofanana na kelele ambazo azina maana kwako. Hata hivyo unajua kwamba hata hiyo lugha ambayo mtu anaweza kujifunza. Mambo kama hayo ndiyo  tunasoma kuhusu imani.

Wakati fulani utagundua wewe ni dhaifu na wakati mwingine mawimbi inakupiga lakini ndani ya moyo wako wa ndani una imani kwamba unaweza tena utaipata kama si hivyo hutathubutu ata kuanza masomo hayo kwa maana hiyo jaribu tu kutembea kwa unyonge, wakati fulani ujasiri tunayo na imani unaanguka unakuwa mazito baadaye tunasalimu amri na kuwacha tunacho fanya.

Tukichoka na kuwacha imani tunayo ni dhambi ambayo hatuwezi kusamehewa tunayo ni dhambi ambayo hatuwezi kusamehewa, mpaka uendelee naye mbele, tena mwezi mmoja ukipita utatoka katika kiwango kimoja ukienda katika kiwango kingine. Muda mrefu ambayo unachukuliwa unategemea katika ugumu wa lugha munayo soma na tena uwezo wa mafunzo na yale wanavyo jitolea kwa masomo hayo- kuta kuwa ma muujiza siki au wakati utafika wewe hujui utagundua ghafla kwamba ulichokitafuta

kimekupata ulichojaribu kukikamata kimekukamata utagundua ghafla ukianza kunzungumza na lugha hiyo iliyo kuwa kama kelele kwako, utafikiri nayo tena kuifahamu. Utagundua kwamba lugha ambayo ilisikika kama kelele msituni sasa itakuwa lugha laini katika fikira yako “Kwa hivyo kuwa katika vita ya imani. Muda au wakati utafika tukijua alama yote tunayopata tukiwa katika mapambano na taaabu unakwisha. Hakika, imani hatuoni tena hatusikii tena. Msururu huu wa imani hatuoni sasa kilicho machoni mwetu ni vitu vingi tunavyo pokea. Tulipo anza kugundua kwamba sisi ni watoto wa Mungu na ukweli wote katika moyo wetu, katika moyowetu tutaanza kujua kwamba mtu wa kale ambaye ni “mimi” una Kristo kama maisha yake ya mbele, moyo na moyo umeungana pamoja ukawa mzabibu; kiungo kimeunganishwa kwa mwili sasa jambo la kuwa Bwana unakuwa rahisi kama kupumua.

Nimeshukuru mwenyezi Mungu kwasababu mahitaji ya moyo ambayo yanajaa hayatasimama mpaka aone ya kwamba mahitaji yake yamekamilika katika maisha yake. Ni kitu ambacho kinahitajika ili tukumbuke mpangilio mkubwa kwa maisha ya moyo yetu. Ya kwamba Mungu anafunua ukweli wa mambo ya Roho ili atimize mahitaji ya Roho. Wangapi wanapumzika katika kiwango cha kwanza cha kuzaliwa upya “kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili si kwa mbegu iharibikayo hali kwa ile isiyoharibika kwa neno la Mungu lenye uzima lidumulo hata milele” (1Pet 1:23) Kuzaliwa mara ya pili kwa mpangilio wa Yesu Kristo unatoka kwa wale waliokufa- hiyo inatufanya tuwe na tumaini mpya. (1 Pet 1:3) Kwa miaka mingi moyo wa mkristo inayoona njaa atajikuta akitoka mbali sana, na tena kila hatua anayo piga katika safari yake ambay ameshakuwa na ujuzi. Ukweli unaotoka katika kuwa na ujuzi. Ukweli unaotoka katika kuwa na imani kwa ukweli wa maneno wa Mungu Wakati tukiingia katika mahitaji ya ukweli kwa imani kwa njia inayofaa, au katika kitu ambacho ni kweli kwetu kwa Kristo tuta gundua kama maneno haya yakifanya kwa undani tena unaoonekana dhahiri tena tabia na mienendo yetu itakamilika katika maisha yetu.

Kwa kweli tutapata tukitoka mbali tukitembea hatua kwa hatua kwa imani. Kupumzika kwa imani kwa kutuweka wenye haki kupumzika kwa imani kwa kutuweka wenye haki kupumzika kwa imani ambayo Mungu anatukubali nayo, kupumzika kwa imani kwa kuchukuwa nafasi yetu kwa Kristo Yesu; kupumzika kwa imani kwa kujitambulisha na Kristo kwa kifo chake, kufufuka kwake tena kupaa kwake akienda mbinguni. Kwa kila hatua tunayopiga tukipumzika kwa imani unatuleta katika hatua nyingine. Kila hatua tunayopiga mpaka ipate nafasi mzuri kabla ya kupiga nyingine.

Hatuwezi kupata maneno yenye nguvu yakuunga nayo mkono kwamba mpaka mkristo ajijenge kwa Warumi 1-5 ndipo anaweza kuingia katika mapumziko yalioko katika Warumi 6-8 haijalishi tumekuwa na mkutano maalum nyingi kiasi gani au kongamano ngapi au mikutano ya (Revivals). Dr. James ambaye anatoka Albany aliyeleta wengi kwa ukweli wa ndani wa maneno ya Mungu aligundua kwamba Mkristo ambaye yuko katika ngazi ya juu amekuwa akianguka katika maisha yake kwa sababu wanasikia maneno na kuyaelewa mpangilio ya injili ya wokovu vibaya. Utagundua kwamba mtu akifundisha atazingatia tu mpango wa kwanzawya mapenzi ya Mungu, na anaweza kuendelea mbele kufundisha mambo mengine zaidi kuzidi kuzaliwa wa pili.

Unaweza kujaribu kujenga maisha ya moyo ambayo hayapo. Utajenga tu yule ambayoamepotea njia kwa maana msingi wa uoko vu wake uliwekwa vibaya. Kama hatuwezi kukaribisha na kushukuru kwa miujiza makubwa ya uokovu ambaye imekamilika kwa Kristo, hivyo basi tutafungua njia ambayo itatufanya tukose amani ambaye itatupa moyo machungu na kutufanya tuanguke.
Wakati mwingi wakristo wengi huweka tumaini yao kwa Mungu kwa jambo ambalo wanalihitaji na wanagundua ghafla wakiteleza wakitoka katika neema wakienda katika mambo ya sheria wakijaribu kuonyesha ukweli fulani ya kazi katika maisha yao.

Tukishapata ukweli ni heri tupumzike na yeye mwenyewe ndiye atatoa mazao, kitu ambacho kinafanyika katika maisha yetu kila siku ni kwamba tukishashika kufunguliwa kwetu ikipitia kifo chetu na Kristo hi vyo basi maisha yetu ya yakipendeza? unaanza kujionyesha ukiwa mzima zaidi- kama zamani? Kama vile Mungu ni Mungu itatupasha tusimame imara tukipumzika kwa maneno yake inayoandikwa. Jambo ambalo litadhihirika ni kwamba kwa kuwa Roho mtakatifu italeta kifo cha msalaba katika kila kitu ambacho ni tofauti na neno la Mungu na inaonyesha kitu ambacho kiko nyuma ya msalaba kwamba mpaka ipelekwe katika msalaba. Kitu ambacho inatupasha kufanya ni kuweka mahitaji yetu kwa Mungu na tena kuwa wakamilifu tukijaribu kufanya mahitaji yetu yawe na uwezo katika maisha yetu. Roho mtakatifu ataweka kifo cha msalaba katika kila kitu kinyume cha Mungu ili iwe kweli kwamba sisi ambao ni wa Kristo tumesulubisha mwili wetu pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake wa Wagalatia 5:24

Imani ambayo inatufanya tupokee vitu kutoka kwa Mungu iko katika vikundi viwili, na tusikufe moyo kwasababu vita na kazi ngumu haijatupatia matokeo mazuri
Mpaka tujuwe kwamba imani inaanza tukiwa watu ambao wanafanya kazi (Wahibrania 4:11) ama wanapiga vita (Timotheo 6:12) ingawa hivyo zinazomezwa zote katika kupumzika (Wahibrania 4:3) Kwa hivyo ninasema ya kwamba hatua ya kwanza ya imani ni kupiga vita tukipata nguvu kwa mahitaji yetu ya kutafuta ukweli wa moyo wetu ya neno la ukweli. Wakati fulani tunaweza kuwa na ahadi yasiyo ya kweli maishani mwetu na tunasema ni yetu hata ingawa inaonekana namna gani. Hatuonekani kama tumekufa kwa dhambi na tu wazima kwa Mungu

Tunaambiwa tuwe na imani kwake kwa hivyo tunajaribu kufanya hivyo tena tunasema tunafanya hivyo. Tuna weza kutukana imani hata mara elfu moja, na tena tutaanguka chii, Moyo ambao hauna imani itasema kwamba hili ni jambo bure tena atakuwa na imani kwa vitu vyake mwenyewe. Na vita tunayopiga ili tuwe na imani inaturudisha kwa matumishi. Na baadaye tunakuwa na imani tena tunasema tuko na imani. Na tukifuata nyayo ya wale ambao wako kwa imani na utulivu utapata nafasi katika maisha yetu kitu ambacho kina utukufu mwema utafanyika katika maisha yetu. Moyo utafanya kazi kisirisiri kila siku). Kwa imani mtaongezewa tumaini ya kweli na kupumzika itachukua nafasi ya vita ambayo itatufikisha pahali ambapo imani inafanya kazi kabisa.

Kazi ya kweli ni ile inafanya na baadaye unawachwa na mapumziko. Ni wakati tutagundua kusimama bila kutingizika ndivyo tutakuwa tayari kuenda mbele. Tunapumzika kwa Mungu tena kwa jina lake tukielekea mbele E H

Wacha tujiadhari, tusipojiadhari tunaweza kutoka nnje ya mapumziko ya moyo yetu tukiendelea kutafuta baraka. Mungu hawezi kuja tukiwa na wasiwasi na tamaa hata ikiwa ni kuwa ma tamaa ya kuwa na ujuzi kwa moyo wetu. Wacha tuchukuwe maneno yake vile vilivyo ili maneno yake yafikishe kazi yake.

# SURA YA 16
# KUMI NA SITA
# USAIDIZI

Wengi wetu wanafaa wawache kuomba Mungu kuwasaidia. Hakutusaidia kupata wokovu, tena hana na nia kutusaidia kuishi maisha yetu ya ukristo.

Yule ambaye hajakomaa kwa Bwana ana hesabu Kristo anamchukulia kama maisha yake mwenyewe. J.E Conant aliandika hivi, kuishi maisha ya ukristo sio kristo akitusaidia, bali ni Kristo mwenyewe ndiye anaishi maisha yake ndani ya maisha yetu. Kwa hivyo maisha aina yoyote ambayo haitatoka kwake haiwezi kuwa kazi ya Kristo. Kwasababu maisha au kazi kama hiyo ni kazi ya binadamu ambayo inatoka kwa nguvu zake na nia zake. Lakini maisha ya kuishi na kutenda kazi kama mkristo inatoka katika nguvu kuu, tena kwa Roho.”mimi nikiwa mzima, uhai wangu ni Kristo nikifa kifo huniletea faida, “Ninaweza kufanya kila jambo kwa ujasiri, kutokana na nguvu ambazo Kristo ananipa’.

Wm R Newell alisema hivi, “kitu amacho shetani anatumia sana kudanganya wateule wa Mungu ni mwenyewe alisema alishatimiza. Kila mmoja wetu anafaa apige hatua kuzidi hatua ya “Usaidizi: kama kuzaliwa kwetu upya na tumshukuru Mungu kwa yale tungefanya wenyewe na akatufanyia

Mungu hawezi kujibu maombi yetu tukimuomba atufanye wenye haki ama tuishi maisha ya Ukristo. Bwana wetu Yesu anangoja ili tumtafute ili tuwe na vitu vyote maishani yetu. Maana katika yeye unakaa utimlifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili, na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka. (Wakolosai 2:9-10)

Hatuwezi tumaini letu kwa Mungu tena hatumpatii heshima anayostahili tukizidi kumwomba ili atusaidie. Tungesema ya kwamba “Mungu atatupa vitu vyote tunavyovihitaji kutoka kwa hazina yake yenye utukufu. Kwa Kristo Yesu, kwa hivyo tunawezaje kuomba usaidizi? kitu tungefanya ni kuona vitu ambavyo ni vyetu kwa neno lake ndani ya Kristo baadaye tunaweka tumaini letu kwake na kumshukuru kwa chochote tunachohitaji. Na hivi karibuni ama kitambo kidogo kulingana na yale F.j Kuegel alisema. Maisha ya Mkristo ya maombi yakitoka pahali panapo faa (ambayo ni nje ya maisha yetu yenye nguvu, kwa Kristo kwa kifo chake tena kwa ufufuo wake) na kutakua na mabadiliko makubwa yanayolingana na neno la Kristo kwa sababu Bwana alisema “ Ombeni na mtapata” lakini kuomba hivyo haifiki mbinguni vizuri kwa kifo na kufufuka kwake: mahali ambapo mtu akifikia atachukua chochote ambacho ni chake kwa kristo. Kasisi Paulo alisema kwamba, “Vitu vyote ni vyenu – na ninyi ni wakristo na Kristo ni wa Mungu. (I Wakorintho3:21-23) Vile- tusipokuwa na imani hatuwezi kufurahisha mungu (Wahibrania 11:6a) Tunaweza kuangalia maneno mengine yenye nguvu tena na ukweli ili tuende mbele tukifafanua namna ya moyo wa kuwa na imani inayofurahisha Mungu.

Wakati tunakuwa na maombi kisirisiri ama katika kazi ya Kristo. Tozer alituandikia hivi, “wakati mwingi tunaomba mungu afanye kitu ambacho tayari a

meshafanya au hawezi kufanya kwa sababu hatuna imani tunamwomba azungumuze na alishazungumza wakati huo anazunguza. Tunamwuomba aje wakati yeye yuko tena anatungoja tumjue.  Tunamwomba Roho mtakatifu atujaze  wakati mwingi tunamzuia kwa sababu tuko na taswishi S.D Gordon anatupa mawaidha hivi, “ukiwa katika vita kuu ambapo watu wengi wanakupiga vita, omba kidogo na upokee nyingi, kwa damu ya Bwana Yesu sineni kwamba uombe Mungu akupe ushindi bali chukua ushindi wake ikufunike.”

Watchman Nee anatujibu hivi, “Njia ya Mungu ya kutoa watu kwa shida ni tofauti na njia ya Binadamu. Njia ya Binadamu inajaribu kuzuia dhambi akijaribu kuishinda. Njia ya Mungu ni kuondoa mwenye dhambi. Wakristo wengi wanalia kuhusu unyonge wao wakifikiria kwamba kama ningekuwa na nguvu zaidi vitu vingekuwa shwari. Nafikiria ambayo iko ni kwamba tusipoishi maisha yetu takatifu tunajichukulia kama watu wajabu, kuna jambo ambalo linahitajika kwetu ili tusiwe na fikra ambayo ya hutuweka huru. Kama nguvu ya dhambi inatuzunguka tena tuna gundua kwamba nguvu tunayo ina upungufu ambao hauwezi kutupa ushindi. Hapo ndipo tutakata kauli tukisema ili tuwe na ushindi juu ya dhambi inatupasa tuwe na nguvu nyingi.
“ Kama ningekuwa na nguvu ningeshinda hasira mbaya iliyonishika “ tunasema hivyo kwa hivyo tunaomba bwana ili atupe nguvu ili tuweze kujilinda, na kitu kama hiki niki baya mno; hii si maisha ya mkristo njia Mungu ya kutufungua na kutuweka huru kutokana na dhambi sio kutuweka wenye nguvu zaidi mbali ni kutuweka wanyonge zaidi.

Kwa ukweli huu ambao ni njia isiyo ya kawaida ya ushindi, wewe unaweza kusema hivyo lakini ndiye njia nzuri. Mungu anatuweka huru kutoka kwa nguvu ya dbambi ikisulubisha mtu wakale na sio kumpatia nguvu na tena sio kumsaidia ili afanye kitu bali akiondoa fikira zake kutoka kwa kile anaweza kufanya”.

Sio vizuri mkristo kuomba usaidizi. Angechukuwa yale yamesha kuwa yake kwa Kristo akishukuru Mungu kwasababu wenye haki wataishi kwa imani (Wahibrania 10:3a) Mpendwa Mzee Andrew Murray anatuhimiza hivi, “hata ingawa njia hii inaenda polepole tena watu hujikwa sana lakini inatufanya tuwe na imani inayotufanya tumshukuru, sio kutokana na ujuzi tunayo maishani mwetu bali kwa sababu ya ahadi aliyotuahidi tunayoweza kutumainia inayoelekea mbele kupata nguvu, kutokana na ukweli wa baraka hii mungu mwenyewe atafanya kazi yake kuwa sana maishani mwetu (Wafilipi 1:6)

## SURA YA 17
## KUMI NA SABA
## KULIMA

Tunaweza kuwa na swali ndogo kuhusu namna inakuwa vyema kuweka vitu viwe katikati vizuri, tena jambo hili lina hitajika kwa aina zote mashine, kazi ya mikono, katika uzuri wa uzito mwingi upande mmoja utaanza kuharibika na mwishowe kuharibu mazingira yake maisha yetu ya kimwili ina uzito upande mmoja, unaegemea upande mmoja kama vile harusi ndogo inayo jumlisha watu wote.

Nilikuwa na harusi ndogo
Jioni moja wakati wa sa tisa
ilikuwa ni sherehe ya watu watatu pekee
walikuwa ni mimi, mimi mwenyewe na mimi pekee.
Mimi alikula kitumbua akampa mimi mwenyewe
Na mimi pekee akanywa chai
Tena mimi alikula kitoweo akampa mimi mwenyewe ugali.

Kwa maana Mungu ni mkulima mkuu akianza kulima moyo wa ukristo alio na njaa ataulima akienda chini. Baba yetu analima akiwa na utulivu akiendelea mbele bila kuwacha tena analima maisha ya kimwili kwa uchungu, tena anajaribu kila mara kutuonyesha hali yetu, na tena hali ambayo hatuna katika maisha yetu. Anatutayarisha hivi kwa maana mbili, ili Yesu apate nafasi katika maisha yetu, tena asaidie wengine kupitia kwetu ili waingie tena wajifunze na wengine pia

Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipo kuwa na majina kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemichemi ambayo maji yake hayapungui (Isaya 58:11)

Mungu mpaka alime kila mmoja wetu zaidi kabla hajaanza kulima wengine kupitia kwetu sio kwamba atutafanya aina yoyote ya kazi mpaka tuwe na ujuzi kwa mambo ya moyo bali ni kwamba kazi yetu nyingi zinazo tupatia ukomavu ni zile zinazotupa ukuaji na sio kwa wengine.

Kwa kuwa neno la Mungu linahitajika kwa mambo ya moyo hivyo basi inahitaji mtu ambaye yuko kwa Roho na itategemea vile Mungu anataka amtumikie mtu huyo: mahali hapa, mtumishi anakuwa na umuhimu kuliko kazi anayoyafanya. Ikilazimika tuwe mkononi mwa Mungu. Atatukiwa katika kazi hiyo atatumikia ili tuongeze thamani ya Roho kwetu.

“Ni makosa kupima ukomavu wetu kwa Roho wakati tu tumeona kupawa. Vitu hivyo hatufai kutazama ili tuwe kwa Mungu milele. Pengine vitu hivyo viko tena vina kazi na kazi muhimu ya Roho ni kuumba Kristo ndani yetu kupitia kwa kazi ya msalaba.

Nia yake kubwa ni kuona Kristo akifanya kazi ndani yetu kupitia kwa wakristo. Kwa hivyo sio kwamba mtu anasema mambo  fulani ama anafanya kazi  fulani. Ni mtu ambaye anahubiri kitu ambacho kiko katika maisha yake.

Watu wengi wanania ya kuhubiri na hao mbele tunapata ya kwamba ni vile tulivyo na tunafanya hiyo ni jambo la muhimu kwa Mungu, tena tofauti ulioko ni kwamba Kristo ameumbwa ndani yetu.

Hatukuumbwa ili tufanye kazi bali tuna kuwa tema kukoma ili tufanye kazi. Ni kama vile kulimwa mwilini kumeonyesha kazi ya mwili kwetu ndivyo hata sisi pia tutakuwa katika kiwango kwetu ndivyo hata sisi pia tutakuwa katika kiwango cha kusaidia wengine wakati wao pia wanalimwa. Tutapata wengine tukishajipata wenyewe. “Kama uso ufananavyo na mwenzake (Mithali 27:19) ili tuweke hekima ya mwili hii katikati Baba yetu anatufanya tu kuwekwa neema tukizidi kumfahamu Bwana yetu Yesu Kris to 2 Pet 3:18)

Jambo hili sio kweli kwa kazi zote tunazozifanya za Mungu, na ni jambo ambalo linahitajika katika huduma mpaka kwa maombi tunayo

Kazi tunayo fanya ya kuchukua jukumu la kuombea wengine inatufanya tuwe na uhusiano nzuri zaidi na Baba, sisi wenyewe na wengine nzuri zaidi na Baba, sisi wenyewe na wengine pia. Kuombea wengine inaweza. Kutokea tu kwa moyo ambao una  utulivu kwa maisha yake mwenyewe, na anafahamu dhamani ya kuwa na nia ya kuchukuwa nafasi kwa watu wengine pia. Kama si hivyo basi hatuwezi kuchukuwa nafasi ya kuomba “Stoney: Paulo aliandika hivi; “Imekuwaje, basi? nitaomba kwa Roho, tena nitaomba kwa akili pia :mtaomba kwa Roho tena nitaomba kwa akili. (2 Wakorinth 14:15)

Wengine wetu wakishaingia ndani ya ukweli ya Bwana basi wataanza kufuruta wengine au kuwashukumu katika, jambo hili la ajabu la ukuaji haraka haraka. Tena wanawalaumu vile wanavyo ua pole pole kwa mafundisho ya maneno haya, tena wanaonekana kama hawana nia ya kuzijia tena hawajali. Tunasahau kwamba muda mrefu unaitajika tena vile tunavyokosa njia jangwani inamfanya Bwana kutembea nasi akipita nasi Jordan akituleta Kanani “Musa alikuwa na hekima yote iliyohitajika ya Misiri na mawazo aliyokuwa nayo ya kuweka waisraeli huru ilikuwa na hekima yote iliyo hitajika ya Misiri na mawazo aliyokuwa nayo ya kuweka waisraeli huru ilikuwa ni kuuwa yule mtu wa Misiri mpaka alifundishawa kwa mambo ya Mungu kwa muda wa miaka arobainne katika nchi ya Midian, lakini alipo tumwa Misiri alimwambia asisumbuke na watu wa Israeli bali aende moja kwa moja kwa Farao aliyewaweka watumwa, Mungu hakuwapatia waisraeli mazoezi kwanza, bali kiongozi ndiye alimpatia taaluma. Mungu anataka kiongozi apewe taaluma kwa mambo ya Mungu” tunavyojifundisha vile Baba yetu anatutumikia kwa muda wa miaka mingi ndivyo hata sisi inafaa tujifunze na wengine.

Mpaka tulimwe ili tulime wengine. Ni jambo ambalo lina umiza ili mkristo alazimishe mkristo mwingine ili apate baraka walakini huyo mtu pengine haukuwa tayari. Kukuwa kwa yule ambaye amelazimishwa inampa adui nafasi ili atudanganye, kwasababu wale ambao wanajaribu kuenda mbio tena wakienda kwa mwendo huo wanajaribu kusukuma wengine, watapata ya kwamba hawawezi kusimama peke yao tena watapata majaribio ambayo hawawezi kuepuka katika ngazi wamejiweka

Tena kilicho cha muhimu ni kwamba kazi ambayo tunayofanya mpaka tuwe na roho sawa. “Tukiwa katika huduma tusitarajia malipo ama faida

karibuni, au vile huduma hiyo ilibadilisha maisha ya huyu ama yule, Jambo la muhimu ni kwamba je kazi hiyo imewekwa mbele ya Mungu na je anaweza kuikubali, na kama anaweza kuikubali tujue ni kipawa ambacho ametupa, “Kwa hivyo, tena, ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa twajitahidi kumpendeza yeye (2 Wakotintho 5:9) watu wengi wanachoka na kuwa bila nguvu wakiona hakuna matunda wanazalisha tena hawawezi kuwa na furaha kama awafanyi kazi. Kazi ni mzuri kiasi, na mpangilio ya kazi ni heri itoke kwa furaha ya kazi hiyo na sio kwamba tufanye kazi ili tuwe na furaha.

Ni heri itoke ndani ya moyo yetu ndani ya nyumba mahali Kristo anaye ushindi na mahali penye nyasi mbichi, mahali upendo unadumu, tena katika kanisa ndiyo mahali mtu anaweza kutokea na kutoa huduma.

Uzuri wa kazi ya mtu itategemea vile Roho ya huyo mtu alivyo pumzika- Tena hiyo utulivu unafafana na vile Mungu pia alivyo pumzika. Ni heri akujue tena akufurahie katika huduma. Tuko na mawaidha madogo kuhusu vile tunavyo onekana kwa nje unavyo onyesha tabia yetu ya ndani. Kama moyo yetu ya ndani haina mapumziko au utulivu basi hatuwezi kutoa huduma tukiwa na utulivu tena tukipumzika; Wakati fulani tunaweza kujaribu tu “J B Stoney.

PS Dalili kubwa ya mapenzi yetu na Kristo ni kulindra watu wake- ukinipenda lisha“kondoo wangu”

**SURA YA 18**
**KUMI NA NANE**
# VILE TUNAVYOWEZA KUENDELEA MBELE

Tukianza mwendo huu wa Mungu tukiwa na moyo yenye njaa tena yenye bidii tutadhani tumepiga hatua kubwa ya maendeleo kama hatujui ya kuwa ndiyo tumeanza. Kama Bwana amesafiri nasi kwa miaka mingi tutagundua polepole kwamba kuna njia yake kubwa tena pana, tena yasio na upeo ya ukuaji ambao ni heri Mungu apite nasi.

Njia hizi za maendeleo ni nchi makavu hakuna kazi ya Roho, hakuna kazi, tunawe kuwa na ushirika na Mungu na wengine kidogo au hatuwezi kuwa nayo hata kidogo wakati mwingine tunaweza kujilazimisha na maombi ama tunaweza kukoma. Chochote tunachofanya itakuwa bure. Wakati inayohitajika kama huu ndivyo mkristo ataona ya kwamba Mungu hayuko naye tena hasaidi tena anaweza kukata kauli asiendelee mbele kwa Mungu. Na hata hivyo katika moyo wake ndani atagundua kwamba ana njaa kubwa ambayo haiwezi kumruhusu awache. “Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama wenye muhuri hii, Bwana awajua walio wake. 2 Timotheo 2:19

Je, vizuri tumpende tena tumtumainie tufanye mapenzi yake ikiwa kuna dalili ya baraka kutoka kwake pekee? Hiyo ni mapenzi ya aina gani? Hiyo ni mapenzi ya ubinafsi? Baba yetu anatoa kila kitu ambacho haistahili kwetu kila mara ili atupe nafasi ya kumpenda, kumtumainia na kufanya mapenzi yake, maana tu yeye ni Baba yetu anajua kile msalaba itafanya katika maisha yetu anajua nafasi ya kifo ambacho kiko mbele yetu ili tuwe na maisha ya ufufuo. Anajua kuwa tasa, mpaka wahubiriwe hata hivyo atatuleta mahali ambapo atutajali yeye ndiye atakuwa muhimu maishani mwetu.

Kuwa mwana ni Muhimu kuliko kuzaliwa upya, unasimamia ukuaji na kuwa mkamilifu. Ni vyema tuwe watoto wakati tuko watoto, Bali ni kitu kibaya kuwa mtoto wakati nafasi ya kuwa mtoto umepita. Na hivi ndivyo wakristo wengi walivyo. Wakati kuwa mwana unaanza katika kuzaliwa upya, agano jipya ina himizo kadhaa zinazotuonyesha kwa kuwa mwana ni kugundua kwamba tumezaliwa. Ni kuwa na ukomavu. Agano jipya himizo nyingi kuhusu ukuaji, tukiacha kuwa watoto na tunakuwa na tabia ya watu wazima.

Katika ukuaji huu tunakuwa na tabia kuu wa Kristo uliokamilika na mali nyingi uliotaka kwa wokovu wetu na tena uliofanya tukaokolewa. “Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu (Warumi 8:19)

Tukianza mwendo huu wa Kristo tutaangalia tu vitu vya nje ya maisha yetu ya ukristo. Lakini Bwana anaruhusu hii kufanyika kwa muda mfupi baadaye ataondoa vitu hivyo ambavyo vinaonekana kwa nnje kwetu ili Bwana Yesu Kristo awe kila kitu katika maisha yetu. Mungu ataanza kutoa vitu ambavyo tulifikiria tunavyo. Baadaye tunaanza mwendo mrefu ya kubeba msalaba tukitoka kwa kufanya tukielekea kwa kupokea.

Mambo ya ukuaji huu ambacho ni cha ajabu mno na isiyo ya kawaida – ambayo ni ukuaji kutoka juu ukielekea chini inaweza kutufanya tufikirie Bwana hayuko nasi tena hatulindi. Hii ni silaha ambayo shetani anakitumia kutudanganya. Ni heri tuone Mungu kama Mungu ambaye ameandikwa katika Biblia ya kwamba yeye ndiye Baba yetu.

Ni kweli kwamba Mungu hachukui watu ambao hawafai kuwaruhusi kunena mambo yake kabla hawajajua kile wataleta. Na sitaki tusimame mahali pamoja. Tunaweza kuendelea mbele kidogo na sio kweli kwamba wakati akaanza kazi yake ya kutunyorosha tena kutuhukumu na tutagundua dhahiri kwamba kile tumekuwa tukisema na kufanya hatujui vizuri. Anatuhitaji tufike katika kiwango ambacho tunaweza kuongea tukiwa na kipawa ama kama hatuna. Kwa sababu katika ujuzi wa maisha ya Kristo ambayo ni vitu vya kiroho ya Mungu sio vitu ambavyo vinaonekana kwa nje kama kipawa bali ni vitu ambavyo vinafanya kazi ndani ya moyo wa mtu unavyoweza kuheshabika. Bwana akianza kuwa kila kitu katika, maisha yetu, au katika vitu tunavyo hivyo basi hata vipawa vyetu havitakuwa muhimu sana maishani mwetu. Hata ingawa tuna fundisha sheria ya maneno haya tena tunavisema na nguvu zake kwa wengine zitakuwa tofauti tofauti kwa sababu Roho mtakatifu ndiye itaendelea mbele kufanya kazi kwa kina maishani mwetu Watchman Nee

Wakati huu mrefu tena mgumu unaweza kutufanya tufe moyo tukiwa na nia ya kuingia mbinguni pekee baada ya kifo na tukihitaji tunayoyatarajia ijumuisha nchi makavu haya yote yatahimiza moyo wetu. Haya yote yatatufanya tuendelee mbele kwa sababu tunajua kwamba wakati wote anaendelea mbele kufanya kazi maishani mwetu kwa kile alicho kianza na kukimaliza ambacho tungeifanya baadaye akatufanyia kwa Yesu Kristo

Moyo wetu ukiwa na ukweli kwake basi tutakuwa na haki kwamba atatuongoza katika hekima ya neno lake kwake haraka, anajua vitu vyote tunavyo weza kusikia ili tuwe na maendeleo, tena hawezi kukosa kutulisha vyakula vinavyostahili na mahitaji yetu wakati huu. Wakati mwingine tunaweza kuona kwamba tutapata nguvu kwa vitu ambavyo havitupatii moyo wa kumpenda kwa sababu tunaona ya kwamba hatuna maendeleo ya haraka tunavyo soma kwa Roho. Tukiangaza macho yetu kwake na tena tunamfuata na moyo wetu wa kawaida akiongoza tutapata ya kwamba anatembea nasi kwa kazi ambazo zitafanya mioyo yetu imkaribishe tena kumshukuru kwake tena kwa vitu vyote vimebarikiwa anayotupatia kwake. Mpaka tuweke tumaini letu kwa upendo wakati wote tujifundishe kindani kwamba sio vizuri kutumainia maisha yetu wenyewe C.A Coates

Paulo anatuandikia hivi, alimuandikia Timotheo

“Basi wewe mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu, na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, kuwafundisha na wengi, ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu 2 Timotheo 2:1-3

Lakini bwana ni mwaminifu atakaye wafanya imara na kuwalinda na yule mwovu 2 Timotheo3:3

Fellowship
BIBLE CHURCH

3217 Middle Road
Winchester, Virginia  22602
540-662-7743
fbc@fbcva.org
www.fbcva.org